Haliuzwi
NOVEMBA 11, 2025
/islamicftz
Jumada I 20 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 557
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Rais awapa ubunge watano, wapigiwa chapuo uwaziri

# Misk ya Roho yarejea baada ya kutofanyika kwa miaka 5

# Dkt. Mwinyi atoa mwelekeo mpya

■ Asisitiza kuwa kudumisha amani, umoja, na mshikamano ni msingi wa maendeleo ya taifa

## Ziara ya BoT Bahrain yaipa sekta ya fedha ya Kiislamu msukumo mpya

Katibu Mkuu wa CIFCA, Bw. Salum Lupande alisema miongoni mwa masuala ambayo taasisi hizo za kimataifa ziliahidi, ni wataalamu, mafunzo jinsi ya kuanza kutumia miongozo katika kuhifadhi na kuripoti mahesabu ya taasisi zinazotoa huduma za Fedha za Kiislamu




Si Uislamu tena...mrengo wa kulia tishio kubwa zaidi la kigaidi Ulaya

# Misk ya Roho yarejea baada ya kutofanyika kwa miaka 5

## Masheikh 'Gen Z' kuipamba kwa mada za amani

Baada ya kupumzishwa kwa miaka 5, kongamano la kila mwaka la Misk ya Roho, linarejea tena mwaka huu Jumamosi ya Desemba 27 katika ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam.

Aref Nahdi, Mwenyekiti wa taasisi inayoandaa kongamano hilo, The Islamic Foundation, alitangaza kurejea kwa kongamano hilo katika mahojiano maalum yaliyorushwa mubashara na TV Imaan, ZBC 2 na Al-Haajar TV ya Kenya.

Nahdi alisema kongamano la mwaka huu litakuwa la kipekee kwani kutakuwa na sura mpya za masheikh lakini pia wengi wao ni vijana.

Nahdi alisema: "Misk ya Roho mwaka huu inawapa nafasi Masheikh vijana. Sio kwamba tunasema masheikh wazee hawafai, hapana. Tunawapa nafasi masheikh vijana ili sisi watu wazima tuwe tunakaa tunaangalia, Je vijana wetu wanafanya sawasawa? Wanapokosea tunaweza tunarekebisha."

Sababu nyingine ya kutumia masheikh vijana, kwa mujibu wa Nahdi, ni kutokana na kauli mbiu ya kongamano hilo isemayo: "Mtume Muhammad (amani ya Allah imshukie na amani), msingi wa amani."

"Tumewapatia masheikh Gen Z kwa sababu Gen-Z wenzao ndio wanaotuletea vurugu. Pengine masheikh vijana wataelewa lugha ya kuzugumza na wenzao. Unaweza kuzungumza mtu mzima, Gen Z wakasema 'Huyu kapitwa na wakati'", alisema Nahdi.

Wakati wa kufunga kipindi, Nahdi alitoa kauli nzito ya kuwaita wapenzi wa da'awah.

"Napenda kuwakaribisha waje. Wale wanaojiandaa na Misk ya Roho ndio wakati wenu. Sasa hivi, tukitoka hapa muanze kuulizia namna ya kupata tiketi msije mkakosa kwa sababu Misk ya Roho ya safari hii ni ya kipekee kabisa. Wadhamini na wafadhili wetu msitutupe mkono tutakuja kugonga milango yenu na inshaAllah mtakuta malipo yenu kwa Allah"

Naye Meneja Mipango wa Kongamano hilo, Idriss Makaka, aliwataja masheikh sita watakaohudhurisha mada katika kongamano hilo kuwa ni pamoja na Sheikh Abdallah AbdulQadir A—Ahdal wa Tanzania atakayejibu swali: 'Je, Mtume Muhammad ni nani?, mada ambayo itawaandalia uwanja masheikh kuja kuogelea katika bahari pana ya mawanda mbalimbali ya amani.

Masheikh wengine ni Sheikh Hassan Muhammadayn pia wa Tanzania atakaelezea Nafasi ya Muislamu katika kulinda Amani; Sheikh Twalib Hassan Ghalib wa Uganda atakayezungumzia Amani ndani ya Familia; na Sheikh Hassan AbdulShakuur wa Rwanda atakayeongelea kuhusu Amani na Uchumi wa Muislamu.

Walinganiaji wengine ni Sheikh Aboubakar Misigaro wa Burundi atakayefafanua Ujumbe wa Amani uliomo katika Qur'an na Sunna na Sheikh AbdulKhaaliq Issa wa Kenya, anayetajwa kuwa ni sheikh kijana zaidi kuliko wote kwa mwaka huu ambaye pia ni rubani wa ndege. Sheikh huyo atakaelezea namna Mtume Muhammad alivyokuwa mfano wa kuigwa katika kulinda amani.

Naye Mkurugenzi wa Makongamano wa The Islamic Foundation, Limbanga Mohamed Limbanga alifafanua kuwa watu 5000 wanatarajiwa kuhudhuria kongamano hilo ambalo kiingilio chake ni Tsh 15,000/= . Alifafanua Waislamu wote, wake kwa waume, wanakaribishwa lakini watoto wa chini ya miaka hawataruhusiwa.

Akihimiza watu kujitokeza kwa wingi, Limbanga alisema Misk ya Roho sio tu ni sehemu ya kupokea da'awah kutoka kwa walinganiaji lakini pia ni fursa ya kutengeneza mtandao wa marafiki wazuri ambao mnaweza kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kadhalika.

Naye Rajab Farjalla, aliyepewa jukumu la kusimamia mauzo na usambazaji wa tiketi amewahakikishia wapenzi wa Misk ya Roho upatikanaji rahisi wa tiketi ikiwemo kuletewa mahali walipo popote Dar es Salaam au mikoani.

# ATN Energies, PGS Security wazungumzia udhamini wao

**Mwakilishi wa ATN Energies, Islam Faraj Huwely, amesema kampuni yao inapenda kuwa sehemu ya kuhamasisha amani, kama kauli mbiu inavyosema.**

Makampuni ya ATN Energies na PGS Security wameelezea kilichowasukuma hadi kujitokeza kudhamini kongamano la Misk ya Roho lililorejea kwa nguvu mpya baada ya miaka 5 ya ukimya.

Akizungumza katika kipindi maalum cha uzinduzi wa msimu wa Misk ya Roho kilichorushwa na TV Imaan, mwakilishi wa ATN Energies, Islam Faraj Huwely, amesema kampuni yao inapenda kuwa sehemu ya kuhamasisha amani, kama kauli mbiu inavyosema.

"Kauli mbiu ya mwaka huu ni amani. Bila ya kuwepo amani sisi wafanyabiashara hatuwezi kufanya biashara zetu. Kutakuwa na vurugu za hapa na pale. Amani ndio imetufanya hata sisi tuweze kuwa mbele hapa tuweze kuzungumza," alisema Huwely.

Alisema amani ni muhimu sana kwa wafanyabiashara hasa kwa maendeleo ya sekta nyeti kama ya mafuta ambayo yanategemewa katika kuendesha viwanda, magari na kadhalika. Kipekee, alielezea kufurahishwa kwake kwamba masheikh ni vijana na watazungumza na vijana ambao bila kupewa msingi wa malezi mema basi mustkabali wa jamii utaharibika.

"Amani ndio kitu cha umuhimu kwa hiyo naomba wafanyabiashara wajitokeze ili kufanikisha Misk ya Roho. Misk ya roho ni moja ya njia za kurejesha kwa jamii. Tutahangaika, lakini jamii ndio muhimu na amani ndio kila kitu,"

Akitoa historia fupi ya ATN Energies, Huwely alisema kampuni hiyo ilianzishwa mwaka 2006 na muasisis wake Abdullatif Twalib Nahdi ambaye ndiye Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mwendeshaji. Alisema tangu ianzishwe, kampuni hiyo imekuwa ikikua hadi kuwa na matawi katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Njombe na kwingineko, na bado inazidi kujitanua.

Kwa upande wake, Fahad Fuad, Mkurugenzi wa PGS Security, amesema kampuni yao inaamini kuwa Misk ya Roho ni jambo la kheri na wao, kama kampuni, ni utamaduni wao kuyakimbilia mambo ya kheri.

Alisema kampuni yake inapodhamini inaangalia faida ambazo watu watazipata kutokana na kongamano hilo kwa kubadilika na kuwasogeza mbele kiimani. Hata hivyo, Fuad pia alisema kudhamini kongamano hilo ni fursa adhimu ya kujitangaza kibiashara. Kampuni ya PGS Security iliasisiwa mwaka 2015 na mwanzilishi wake Ahmed Omar Bawazir.

**KUTOKA MAKTABA:** Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, Mufti wa Zanzibar Sheikh Omar Al Kaab na Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi katika matukio ya makongamano yaliyopita ya Misk ya Roho

NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi atoa mwelekeo mpya

## Asisitiza kuwa kudumisha amani na umoja ni msingi wa maendeleo ya taifa

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, Jumatatu Novemba 10, 2025, alizindua rasmi Bunge la 11 la Wawakilishi, akieleza vipaumbele vikuu na mwelekeo mpya wa serikali yake kwa muhula wa pili, huku akiahidi kuendeleza maridhiano na kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU).

Dk. Mwinyi alisema serikali mpya italenga kuimarisha nidhamu, uzalendo, weledi na uadilifu, sambamba na kukabiliana na vitendo vinavyodhoofisha utawala bora.

Akilihutubia Bunge hilo Jumatatu, Dk. Mwinyi alisema serikali atakayounda inalenga kusukuma mbele mipango mikubwa ya maendeleo na kuimarisha mafanikio yaliyopatikana katika muhula wake wa kwanza.

Alisema serikali ya muhula wa pili itahakikisha ukuaji wa uchumi unasukumwa na sekta za uzalishaji, ongezeko la fursa za uwekezaji, upatikanaji bora wa mitaji, na ushiriki thabiti wa sekta binafsi.

"Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa, serikali itadhibiti mfumuko wa bei usizidi asilimia tano kwa mwaka, kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) kutoka asilimia saba hadi 10 kwa mwaka, kuunda ajira mpya 350,000, na kuongeza kipato cha kaya," alisema.

### Amani na umoja wa kitaifa

Katika hotuba yake ya dakika 50, iliyotolewa kuanzia saa 5:35 asubuhi hadi 6:25 mchana, Dk. Mwinyi alisisitiza kuwa kudumisha amani na umoja ni msingi wa maendeleo ya taifa.

"Ni dhamira yangu ya dhati kuendelea kuwaunganisha Wazanzibari bila kujali kabila, dini, jinsia, asili au itikadi ya kisiasa," alisema.

Aliahidi kuwa uwiano na ushirikishwaji vitazingatiwa katika uteuzi na upatikanaji wa fursa za ajira katika utumishi wa umma.

"Nitaheshimu roho ya maridhiano na niko tayari kuitekeleza kupitia uundaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU) kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984," alitangaza.

### Utumishi wa umma na uadilifu

Dk. Mwinyi alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa umma kwa kuwapatia mafunzo, zana za kazi na motisha bora ili kuongeza ufanisi.

"Tutaimarisha uzalendo, nidhamu na uwajibikaji ndani ya utumishi wa umma kwa kuimarisha mifumo inayohakikisha uadilifu, maadili na utendaji kazi bora," alisema.

Aliongeza kuwa Ofisi ya Usalama wa Uendeshaji wa Serikali (GOS) itaratibu na kufuatilia nidhamu katika taasisi za umma ili kuhakikisha uwajibikaji unakuwa utamaduni endelevu.

Rais alisisitiza kuwa serikali itaendelea kupambana na rushwa, ubadhirifu wa uchumi, na mienendo isiyo ya kimaadili katika utumishi wa umma.

### Uchumi wa buluu

Dk. Mwinyi alisema serikali katika muhula wa pili itaongeza kasi ya kukuza uchumi wa buluu.

"Serikali inapanga kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar kutoka 800,000 hadi milioni 1.5, na kuongeza matumizi ya wastani kwa kila mtalii kwa siku kutoka dola 418 hadi 506. Pia tunalenga kuongeza wageni wanaotembelea Pemba kutoka 200,000 hadi 300,000," alisema. Alitangaza mpango wa kujenga bandari mbili kubwa za uvuvi — Ngalawa (Unguja) na Shumba Mjini (Pemba) — na kununua meli za kisasa za uvuvi.

### Sekta za uzalishaji

Akiongeza umuhimu wa kilimo kwa usalama wa chakula na maisha ya vijijini, Dk. Mwinyi alisema serikali itaboresha sekta hiyo kwa teknolojia na mageuzi ya kimuundo.

"Serikali itaanzisha hifadhi ya chakula ya taifa kwa kukarabati maghala manne na kujenga vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 kwa wakati mmoja," alisema.

Aliongeza kuwa mifumo ya kidijitali itaanzishwa kurahisisha usajili wa vyama vya ushirika, kuhakikisha masoko ya uhakika, na kuhamasisha vyama hivyo kuwekeza katika Benki ya Ushirika Tanzania.

### Miundombinu

Dk. Mwinyi alisema miradi mikuu ya usafiri itahusisha ujenzi wa barabara za Tunguu–Makunduchi (km 48), Fumba–Kisauni (km 12), Mkoani–Chake (km 43.5), na barabara za kufikia maeneo ya utalii Nungwi (km 12).

Aidha, idadi ya abiria wanaopita viwanja vya ndege vya Zanzibar inatarajiwa kuongezeka kutoka milioni 2.14 hadi milioni 2.82 ili kuongeza mapato na ajira.

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Ziara ya BoT Bahrain yaipa sekta ya fedha ya Kiislamu msukumo mpya

Juhudi za Tanzania kuijenga hadi kufikia viwango vya kimataifa sekta ya fedha inayofuata misingi ya Sharia zimepata msukumo mpya baada ya taasisi mbili kubwa za miundombinu ya fedha ya Kiislamu duniani, kila moja kwa wakati wake, kuahidi kushirikiana kwa hali ya juu na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kuimarisha sekta hiyo nchini.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika vikao vya pande mbili kati ya ujumbe wa BoT na Shirika la Uhasibu na Ukaguzi kwa Taasisi za Fedha za Kiislamu (AAOIFI) na baadae Wakala wa Kimataifa wa Kutathmini Shughuli za Fedha za Kiislamu (IIRA). Vikao hivyo vilifanyika pembeni ya Kongamano Kuu la Kimataifa la Wadau wa Mfumo wa Fedha unaofuata Sharia lililofanyika nchini Bahrain Novemba 2 hadi 3, 2025.

Akiongea na Gazeti Imaan, Katibu Mkuu wa Kituo cha Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri (CIFCA), Bw. Salum Lupande, ambaye pia ni Mkaguzi na Mshauri wa masuala ya Fedha yanayofuata misingi ya Kiislamu aliyethibitishwa na AAOIFI (AAOIFI Certified Shariah Auditor and Advisor) aliyeshuhudia majadiliano hayo nchini Bahrain, alisema mafanikio makubwa yamepatikana kupitia vikao hivyo.

Lupande alisema miongoni mwa masuala ambayo taasisi hizo za kimataifa ziliuahidi ujumbe huo wa BoT ulioongozwa na Bw Beatus Adrian Rwegalulira, Mkuu wa Kitengo cha Leseni na Sera akiongozana na Bi. Zuwena Salim Soud, Mkaguzi wa Mabenki, ni wataalamu wa AAOIFI kuwasilisha mafunzo ya mwongozo kwa Tanzania kuhusu jinsi ya kuanza kutumia miongozo ya shirika hilo katika kuhifadhi na kuripoti mahesabu ya taasisi zinazotoa huduma za Fedha za Kiislamu.

Katika vikao hivyo na ujumbe wa BoT, shirika la AAOIFI lililowakilishwa na Katibu Mkuu wake, Bw. Omar Mustafa Ansari, pia limekubali kutoa wataalamu wa kupitia na kutoa maoni juu ya rasimu ya muongozo wa Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania kwa taasisi zinazotoa huduma za fedha zisizokuwa na riba. Hatua hii inatarajiwa kusaidia kanuni za Tanzania zilingane na viwango vya kimataifa.

Pia, AAOIFI waliahidi kuleta wawakilishi wao katika Kongamano la Mwaka la Mfumo wa Fedha wa Kiislamu Tanzania lililopangwa kufanyika Jumamosi Januari 31, 2026 chini ya uandalizi wa CIFCA kwa kushirikiana na wadau wengine katika sekta hii, jambo linaloonyesha kutambuliwa na kuthaminiwa kwa jitihada za Tanzania katika sekta hii.

Kwa upande wa IIRA, taasisi hiyo imeonesha nia ya kuanzisha ofisi au kuingia mkataba wa makubaliano na taasisi ya Tanzania ili kuweza kutoa huduma za uwezeshaji na tathmini katika soko la mitaji Tanzania. Ili kufaikisha hilo, na mengine, uongozi wa IIRA umeahidi kutembelea Tanzania wiki ya pili ya mwezi Januari 2026 kwa ajili ya kuhakiki na kuandaa mazingira ya mashirikiano na utoaji huduma zao ndani ya Tanzania na nchi za jirani.

Kupatikana kwa chombo cha tathmini cha Kiislamu, inategemewa, kutasaidia kuongeza uwazi, uaminifu na kuvutia wawekezaji wa Kiislamu katika miradi ya ndani.

Ikumbukwe kuwa, hata kabla ya ziara hii ya ujumbe wa BoT nchini Bahrain, tayari kumekuwa na ushirikiano wa karibu kati ya mashirika hayo ya kilimwengu na Tanzania kupitia CIFCA.

Mathalan, mnamo mwaka 2021 AAOIFI waliingia mkataba na CIFCA wa kuratibu uwezeshaji wa watalaamu katika sekta ya mfumo wa fedha wa Kiislamu ambapo wataalamu wengi wa Kitanzania wamenufaika. Katika ziara hii, AAOIFI wameuthibitishia ujumbe wa BoT kuwa wataendelea kushirikiana na CIFCA.

Aidha, AAOIFI waliujulisha ujumbe wa BoT kuwa mipango ilikuwa imekamilika ya kusaini mkataba wa maridhiano na Amana Benki na CIFCA wa kutafsiri miongozo ya AAOIFI kwenda katika lugha ya Kiswahili kama sehemu ya vikao vya pembeni vya kongamano hilo. Kwa bahati mbaya, timu ya Amana Benki ilishindwa kusafiri kwa sababu ndege yao ilisitisha safari kutokana na machafuko ya kisiasa yaliyotokea baada ya Uchguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025.

IIRA, nayo, kama AAOIFI ina mkataba kama huo wa ushirikiano na CIFCA uliosainiwa nchini Bahrain tangu mwaka 2021. Katika makubaliano hayo, CIFCA iliwakilishwa na Mwenyekiti wake, Bw Aref Nahdi ambaye amekuwa mhimili muhimu katika mafanikio ya CIFCA kutokana na miongozo yake na kujitolea kwa hali na mali, kupitia taasisi yake ya The Islamic Foudation, ili kuhakikisha sekta ya fedha ya Kiislamu inakua na kuimarika hapa nchini.

## Kongamano lilivyofana

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu Lupande, Kongamano hilo la kimataifa lililoandaliwa kwa pamoja na AAOIFI na Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB) lilifanyika kwa mafanikio makubwa likiwakutanisha wataalamu, wasimamizi wa fedha, wanazuoni wa Shariah, na wadau wa sekta ya Fedha ya Kiislamu kutoka duniani kote.

Mada kuu ya kongamano hilo ilikuwa ni mabadiliko ya kiuchumi duniani na athari zake kwa taasisi za fedha za Kiislamu, hususan kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya Akili Mnembe (Artificial Intelligence – AI) katika nyanja mbalimbali za biashara na ufuatiliaji wa Shariah.

Pamoja na kuhudhuria Kongamano Kuu hilo, washiriki walipata pia nafasi ya kushiriki katika Wiki ya Ujenzi wa Uwezo wa Wadau wa Mfumo wa Fedha ufuatao Shariah (AAOIFI Capacity Building Week – CBW) iliyoanza Novemba 1 hadi Novemba 7 huko huko nchini Bahrain yakiandaliwa na na Taasisi ya Benki na Fedha ya Bahrain (BIBF) ikishirikiana na AAOIFI.

Mafunzo haya yalilenga kuimarisha ujuzi wa wataalamu katika sekta ya fedha za Kiislamu kwa kuzingatia zaidi utekelezaji wa viwango vya AAOIFI. Washiriki walipata maarifa ya vitendo kuhusu mbinu bora za kimataifa, mahitaji ya kisheria, na maendeleo mapya katika sekta hii, yote yakiwa yamepangwa kwa mujibu wa viwango vya AAOIFI. Mafunzo haya yalitarajiwa kuwapatia washiriki ujuzi na umahiri unao-

# Ziara ya BoT Bahrain yaipa sekta ya fedha ya Kiislamu msukumo mpya

hitajika ili kuongeza ufanisi na mchango wao katika majukumu wanayoyatekeleza ndani ya taasisi zao.

Sehemu ya tatu ya programu ilijumuisha ziara ya kitaalamu katika taasisi zinazounda mnyororo wa thamani wa fedha za Kiislamu nchini Bahrain ikiwa ni fursa ya wageni kujifunza mifumo iliyofanikiwa na kupeleka makwao, ikiwemo Tanzania.

Kwa siku zilizobakia za ziara (Jumapili tarehe 9 mpaka Ahamisi tarehe 13/11/2025), wawakilishi wa BoT, chini ya ushirikiano na wenyeji AAOIFI wamepanga kuwafikia washiriki wengine katika sekta ya fedha ya Kiislamu wakiwemo.

Wadau ambao ujumbe wa BoT unatarajia kukutana nao ni pamoja na Benki Kuu ya Bahrain, mabenki yanayoufuata mfumo wa Kiislamu kwa asilimia 100, mabenki yenye madirisha yanayotoa huduma za fedha za Kiislamu, watoa mafunzo mbalimbali wa elimu ya mfumo wa fedha wa Kiislamu, watunga sera na mashirika ya wakaguzi wa kimataifa wa mahesabu ya taasisi zinazotoa huduma za fedha za Kiislamu.

Lupande amesema lengo la kukutana na wadau hao ni kukamilisha uelewa wa namna ikolojia ya mfumo wa fedha wa Kiislamu inavyofungamana katika kuhakikisha huduma na bidhaa zote muhimu zinatolewa kwa ufanisi mkubwa nchini Bahrain, na kuweza kujifunza mbinu za kuunganisha mfumo huo kwa Tanzania kwa mafanikio mapana zaidi.

## Tanzania yasifiwa

Kwa mujibu wa Bw. Lupande, wadau wa kimataifa waliisifu Tanzania kwa kupeleka chombo kikuu cha usimamizi wa sekta (regulator) kwenye kongamano hilo la kiwango cha juu, na waliwatumia kama mfano kwa nchi nyingine – kwamba ili mfumo wa fedha wa Kiislamu ukue, benki kuu lazima iwe mstari wa mbele.

Kwa upande wa Tanzania, hatua hizi zinafungua njia ya kuwa na kanuni zilizo wazi, hatifungani (sukuk) zinazokubalika kimataifa, mafunzo yenye viwango vya kimataifa na hatimaye bidhaa nyingi zaidi za Kiislamu kutoka mabenki, Takaful na masoko ya mitaji. Kwa ujumla, maafikiano haya yanaweka Tanzania kwenye nafasi ya kuharakisha "Islamic finance roadmap" yake, kwa sababu sasa benki kuu, mashirika ya viwango vya kimataifa na wakala wa tathmini wanasogea pamoja, kila mmoja akijua jukumu lake: BoT kuweka kanuni, AAOIFI kutoa mwongozo wa shariah na uhasibu, na IIRA kuongeza uaminifu wa soko kwa tathmini huru.

# HABARI DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Rais Samia adokeza majina ya mawaziri watarajiwa kufuatia wabunge wapya aliowateua

Rais Samia Suluhu Hassan jana aliteua Wabunge wapya sita, hatua inayoweza kuashiria baadhi ya majina yanayotarajiwa kuingia katika baraza lake la mawaziri lijalo.

Uteuzi huo, ambao unaanza mara moja, ulitangazwa kupitia taarifa ya gazeti la serikali iliyotolewa na Ofisi ya Rais Ikulu Dodoma. Taarifa hiyo, iliyosainiwa na Katibu Mkuu Moses Kusiluka, ilirejelea Kifungu cha 66(1)(e) cha Katiba, kinachompa Rais mamlaka ya kuteua Wabunge hadi kumi.

Wateule wapya ni miongoni mwao mawaziri wa zamani, mabalozi na wasimamizi, ikionyesha upendeleo wa Rais Samia kwa watu wenye uzoefu katika utawala na sera.

Miongoni mwa wateule ni Dk. Dorothy Gwajima, daktari wa tiba na aliyekuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu. Pia amewahi kuwa Waziri wa Afya na Naibu Katibu Mkuu wa Kudumu katika Ofisi ya Rais (Utawala wa Mkoa na Serikali za Mitaa).


Dk. Bashiru Ally

Mahmoud Thabit Kombo

Dk. Bashiru Ally, mtaalamu wa elimu, balozi na mkakati wa kisiasa, pia anarudi kwenye jukwaa la kisiasa. Ni aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa chama tawala Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wabalozi wengine wawili wenye uzoefu, Mr. Mahmoud Thabit Kombo na Mr. Khamis Mussa Omar, pia wako kwenye orodha. Mr. Kombo amemaliza hivi karibuni muda wake kama Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Rais pia ameteua Mr. Abdullah Ali Mwinyi, kiongozi wa biashara na mwana wa Rais wa zamani Ali Hassan Mwinyi, pamoja na Dk. Rhimo Nyansaho, ambaye amewahi kuhudumu katika bodi kadhaa muhimu, ikiwemo kama mwenyekiti wa Tanzania Electric Supply Company Limited (Tanesco).

Wachambuzi wanasema uteuzi huu unalingana na mkakati mpana wa Rais Samia wa kuimarisha utawala wake kwa mchanganyiko wa wataalamu, wabalozi na wanasiasa wenye uzoefu, huku akijiandaa kwa mabadiliko yanayoweza kufanyika katika Baraza la Mawaziri.

# Pongezi kwa Rais Samia zamiminika, aahidiwa ushirikiano

Viongozi mbalimbali wa bara la Afrika na dunia wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kuongoza Tanzania, wakiahidi kuendeleza na kuimarisha ushirikiano wa kisiasa, kiuchumi na kijamii na nchi hiyo katika kipindi chake kipya cha uongozi.

Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) ilimtangaza Rais Samia mshindi wa uchaguzi mkuu wa Oktoba 29, 2025 baada ya kupata kura 31,913,866 sawa na asilimia 97.66 ya kura zote zilizopigwa kati ya wapiga kura waliosajiliwa milioni 37.6, hatua iliyothibitisha kwa mara ya kwanza kuchaguliwa kwa wadhifa alioukalia tangu 2021 kufuatia kifo cha Dkt. John Magufuli.

Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AU), Mahmoud Ali Youssouf, katika taarifa yake ya Novemba 1, 2025 alitoa pongezi kwa Rais Samia na watu wa Tanzania, akisisitiza kwamba AU iko tayari kuendelea kuiunga mkono nchi hiyo katika kulinda amani, mshikamano wa kitaifa na mchakato wa kidemokrasia.

Hata hivyo alisikitishwa na vifo vilivyoripotiwa kufuatia maandamano ya baada ya uchaguzi na kuwataka raia na mamlaka kuheshimu haki za msingi, uhuru wa kujieleza na kujikusanya kwa mujibu wa sheria, sambamba na kanuni za Mkataba wa Afrika juu ya Demokrasia, Uchaguzi na Utawala.

Kutoka eneo la Afrika Mashariki, Rais wa Kenya William Ruto na mwenzake wa Uganda Yoweri Museveni walituma salamu za pongezi wakisema ushindi wa Rais Samia unaonesha imani ya Watanzania kwa uongozi wake na kwamba nchi zao ziko tayari kuendeleza ushirikiano wa kibiashara, miundombinu na ujumuishaji wa kikanda kupitia EAC.

Rais Ruto aliwataka wadau wote wa siasa nchini Tanzania kutilia mkazo mazungumzo na kuhifadhi umoja wa taifa baada ya uchaguzi.

المؤسسة الإسلامية

The Islamic Foundation

Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation ***Aref Nahdi*** anampongeza ***Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan*** kwa Kuaminiwa na kuchaguliwa na Watanzania kuendelea kuwa Rais wa awamu ya sita wa Jamuhuri ya muungano wa Tanzania.

**IMAAN DIGITAL**

**www.islamicftz.org**

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Dhahabu na mazao ya kilimo yaongoza ukuaji wa mauzo ya nje ya Tanzania

Mauzo ya bidhaa na huduma kutoka Tanzania yameendelea kupanda kwa kasi, yakiongezeka kwa takribani asilimia 15 hadi kufikia dola bilioni 17.09 katika mwaka ulioishia Septemba 2025, kutokana na ongezeko la mapato kutoka kwa dhahabu, bidhaa zilizotengenezwa viwandani, na mazao ya kilimo ya kiasili.

Kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ukuaji huo umetokana na mapato makubwa yaliyotokana na dhahabu, bidhaa za viwandani, na mazao ya kilimo ya kiasili — hususan korosho na tumbaku — pamoja na kuongezeka kwa mapato ya huduma kutoka sekta za utalii na usafirishaji.

“Ukuaji huu umetokana kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mapato ya huduma pamoja na utendaji mzuri katika mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, na mazao ya kiasili kama korosho na tumbaku,” taarifa ya BoT ilisema.

Mauzo ya bidhaa nje yaliongezeka kwa kasi hadi dola bilioni 10.12, kutoka dola bilioni 8.23 mwaka ulioishia Septemba 2024. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, korosho, nafaka, na tumbaku.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mauzo ya dhahabu yalipanda kwa asilimia 35.8 hadi dola bilioni 4.43, kutoka dola bilioni 3.26 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita — jambo linaloonyesha ongezeko la bei ya dhahabu duniani na uzalishaji thabiti. Dhahabu iliendelea kuwa chanzo kikubwa zaidi cha fedha za kigeni nchini, ikichangia takribani asilimia 44 ya mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi.

Mauzo ya mazao ya kiasili pia yaliongezeka kwa kasi, yakifikia dola bilioni 1.48, kutoka dola bilioni 1.07 mwaka uliopita — sawa na ongezeko la asilimia 38.3. Ukuaji huu ulitokana hasa na utendaji mzuri wa korosho na tumbaku, ambazo zilinufaika na bei nzuri za kimataifa na ongezeko la kiasi cha mauzo.

Mauzo ya korosho karibu yaliyoongezeka mara mbili, kufikia dola milioni 527.6, ikilinganishwa na dola milioni 225.6 awali, huku mauzo ya bidhaa za viwandani yakipanda kutoka dola bilioni 1.3 hadi dola bilioni 1.56.

Thamani ya mauzo ya nafaka nayo iliongezeka maradufu hadi dola milioni 340.6, kutoka dola milioni 194.2 mwaka 2024. BoT imeeleza kuwa ongezeko hilo limechangiwa na mahitaji makubwa kutoka nchi jirani kama Kenya, Rwanda, na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Bidhaa zilizotengenezwa viwandani ziliendelea kufanya vizuri kutokana na ukuaji wa sekta ya viwanda na uimarishaji wa masoko ya kikanda. Ripoti inaonyesha kuwa mauzo yasiyo ya kiasili — hasa dhahabu, bidhaa za viwandani, na mazao ya bustani — yameendelea kuwa nguzo kuu ya mapato ya nje ya nchi.

Kwa mwezi mmoja, mauzo ya bidhaa nje yalifikia dola bilioni 1.02 mwezi Septemba 2025, kutoka dola milioni 934.2 mwezi kama huo mwaka 2024, yakichochewa zaidi na dhahabu na bidhaa za viwandani.

Wakati huo huo, mapato ya huduma yaliongezeka hadi dola bilioni 6.97 katika mwaka ulioishia Septemba 2025, kutoka dola bilioni 6.67 mwaka uliopita — ongezeko la asilimia 4.6. Ukuaji huu umetokana zaidi na mapato kutoka huduma za utalii na usafirishaji, ambazo kwa pamoja zinachangia sehemu kubwa ya mapato ya huduma.

Takwimu za BoT zinaonyesha kuwa mapato kutoka sekta ya utalii yameendelea kuimarika, yakionesha urejeo thabiti wa sekta hiyo huku idadi ya watalii ikiongezeka kwa asilimia 11.9 hadi wageni 2,315,637. Ripoti inabainisha kuwa ongezeko hilo limechangiwa na kampeni za utalii na uimarishaji wa miunganisho ya safari za ndege.

Vivyo hivyo, mapato ya huduma za usafirishaji — hasa mizigo — yalipanda hadi dola bilioni 2.54, kutoka dola bilioni 2.28 mwaka uliopita, yakichangiwa na ongezeko la biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki. Hata hivyo, kwa mwezi mmoja, mapato ya huduma yalishuka kidogo hadi dola milioni 576 mwezi Septemba 2025, kutoka dola milioni 584.7 mwaka uliopita, kutokana na mabadiliko ya msimu.

Upande wa uagizaji, ripoti inaonyesha kuwa uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka hadi dola bilioni 17.73 katika mwaka ulioishia Septemba 2025, kutoka dola bilioni 16.76 mwaka uliopita. Ongezeko hilo limechangiwa na uongezekaji wa vifaa vya viwandani, mitambo, sehemu na vifaa vya magari, pamoja na vifaa vya usafiri.

Hata hivyo, uagizaji wa mafuta — ambao unachangia takribani asilimia 16.8 ya uagizaji wote — ulipungua hadi dola bilioni 2.47, kutoka dola bilioni 2.75 mwaka uliopita, kutokana na kupungua kwa bei za mafuta duniani.

MAKALA MAALUM

NA SHEIKH SHAABAN MUSSA

# Mitandao ya kijamii itumike kuleta maendeleo, kulinda amani

Katika uchaguzi wa 2020, mitandao ya kijamii iligeuka uwanja wa kelele, umbea, tetesi, matusi na jazba huku video, vichekesho na maandiko yakitumika kudhalilisha watu na hata taifa.

Kulijitokeza makundi ya mtandaoni—mengine yakiwa na sura za watu wanaofahamika, mengine yakiwa na majina ya kuficha—lakini yote yakitumia hasira za watu kuchochea mfarakano, uharibifu wa mali na chuki za kisiasa.

Matokeo yake, tukajikuta na jamii iliyogawanyika: upande mmoja waliokuwa wakikosoa kwa lugha isiyo na mipaka; wengine wakijibu kwa ukali uleule bila kujali sheria wala utu.

Mwaka huu, 2025, kasi hiyo iliongezeka; taarifa potofu, picha za vurugu na kauli za kuchochea zimefanya majukwaa ya kidijitali yaonekane kama tanuri la kuoteshea ghasia badala ya jukwaa la hoja.

Onyo la Qur'an na Hadith

Uislamu haukuacha uwanja wa maneno bila mwongozo. Allah anasema: "Wala usifuatilie jambo usilolijua. Hakika kusikia, kuona na moyo vyote hivyo vitasailiwa." [Qur'an,17:36]. Na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) akasema: "Inamtosha mtu kuwa muongo anaposema kila anachosikia." [Muslim]. Machapisho ya mtandaoni yako kwenye hukumu hii hii: ukishiriki bila kuthibitisha, unakuwa sehemu ya tatizo. Uislamu unatuitia subira, hekima na uadilifu—si dhihaka, si uchochezi.

## Athari za kijamii

Wanasaikolojia wanasema kurudiakurudia lugha ya chuki mtandaoni kunamfanya mtu aione kama njia halali ya kutatua tofauti. Mitandao huweza kumgeuza mtu mnyenyekevu kuwa mpinzani mkali wa mfumo, akihamasisha ghasia kwa jina la haki. Na hiki ndicho kilichotokea.

Qur'an inatuonya: "Wala chuki ya watu isikuchocheeni kutokutenda haki. Fanyeni uadilifu; hakika uadilifu unakaribia mno na uchamungu." [Al-Maida 5:8].

Aya hii inasisitiza kuwa katika mazingira yoyote, uadilifu na uchamungu vinapaswa kutangulia hisia, hasira na mihemko yetu. Kwa hiyo, hata tukipishana katika maoni, Uislamu unatuita tuwe na adabu na hekima. Maneno mazuri ni silaha ya amani; maneno mabaya ni cheche ya moto na mfarakano.

## Kuimarisha ulinzi wa kijamii na kidijitali

Ni wajibu wa jamii nzima kuhakikisha mitandao inabaki kuwa chombo cha elimu, uwazi na maendeleo si jukwaa la kuchochea ghasia au migawanyiko ya kidini na kijamii kwenye jamii.

Kwa muda mfupi, mamlaka ziimarishe ufuatiliaji wa maudhui za uchochezi, na kushirikiana na majukwaa ya mitandao ya kitaifa na kimataifa katika kuondoa maudhui zilizokiuka sheria na maadili.

Kwa muda wa kati, tuwekeze katika elimu ya kidijitali yaani uwezo wa mtu kutumia, kuelewa, kuchambua na kutathmini taarifa zinazopatikana kwenye tovuti na mitandao ya kijamii na kung'amua habari potofu na hivyo kutumia mitandao kwa uwajibikaji zaidi.

Kwa muda mrefu, jamii inapaswa kujenga utamaduni wa kuvumiliana kisiasa, kuweka sheria kudhibiti matumizi mabaya ya mitandao, na kuimarisha miundombinu ya kidijitali yenye uwezo wa kustahimili mashambulizi na upotoshaji.

Hatua za Muda mfupi (saa hadi wiki): kuchunguza vikundi vinavyopotosha maadili na kuhamasisha vurugu mtandaoni sambamba na kuzuia maudhui yenye vitisho na kutoa ujumbe wa utulivu. Pia, tufungue njia rahisi za kuripoti maudhui hatarishi.

Muda wa kati (mwezi 1–12): Tuimarishe timu za ulinzi wa mtandao na kutoa mafunzo kwa vyombo vya sheria kuhusu ushahidi wa kidijitali. Pia, tuhamasisha vijana, waandishi wa habari na viongozi wa mitaa kuhusu matumizi salama ya mitandao sambamba na kuingia makubaliano na kampuni za mitandao ili kudhibiti maudhui ya uchochezi.

Muda mrefu (mwaka 1–5): Turekebishe sheria ili kulinda uhuru wa kujieleza na kudhibiti chuki. Tujenge imani ya kijamii kupitia elimu ya uraia, mijadala ya amani na huduma za kijamii. Pia, tuimarishe miundombinu ya kidijitali ya taifa ili kupunguza athari za mashambulizi makubwa.

Nihitimishe kwa kumnukuu Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) aliyesema: "Muislamu hasa ni yule ambaye Waislamu wengine wako salama kutokana na ulimi wake na mikono yake." [Sahih al-Bukhari na Muslim].

Katika zama hizi za teknolojia, "ndimi" zetu ni vidole na machapisho ya mtandaoni. Tukiitumia teknolojia kwa hekima, tutajenga taifa lenye umoja, uwazi na amani, lakini tukizitumia kueneza chuki, tutapotea na kujipoteza sisi wenyewe.

Iwe dira kwa kila raia Qur'an inayotuhimiza: "Na semeni na watu kwa wema." (Surat Al-Baqarah, 2:83). Kila chapisho, kila maneno tunayoshiriki, vinaweza ama kujenga amani au kuvuruga umoja. Ni jukumu letu kuchagua busara, kama walivyosema wahenga wa kale: "Kalamu ni amana; usiitumie kuumiza."

Kwa pamoja, tukiweka maadili haya mbele, tutaweza kugeuza kelele za mitandaoni kuwa sauti za maendeleo na ujenzi wa demokrasia yenye afya, inayolinda miundombinu, utu na heshima ya kila mwanadamu.

NA MWANDISHI WETU

# Dkt Nchimbi aashiria ujio wa maaridhiano

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Emmanuel Nchimbi, amewahakikishia viongozi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwamba Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan imejipanga kikamilifu kukamilisha mchakato wa maridhiano ili nchi iendelee kubaki tulivu, yenye umoja na mfano wa amani barani Afrika.

Dkt Nchimbi alitoa kauli hiyo akimwakilisha Rais Samia katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika kwa njia ya mtandao wakati akiwa Dodoma.

Alisema Tanzania bado iko salama na shwari, na inaendelea kuwa tayari kupokea wageni, wawekezaji na watalii kutoka pande zote duniani kwa manufaa ya nchi wanachama wa SADC na Afrika kwa ujumla.

"Tanzania ni salama na inaendelea kuwa mwenyeji wa wageni kutoka duniani kote. Serikali yetu inaendelea kuupa kipaumbele mchakato wa maridhiano ili tuendelee kuwa taifa moja, imara na lenye kuaminika," alisema Dkt Nchimbi.

Mkutano huo pia ulimpongeza Rais Samia kwa ushindi alioupata katika uchaguzi wa hivi karibuni, wakisema ni ishara ya kuendelea kuaminiwa na Watanzania na kwamba utaendeleza uhusiano mzuri kati ya Tanzania na nchi jirani ndani ya jumuiya.

Aidha, viongozi hao walikubaliana kuendeleza kaulimbiu ya Mkutano wa 45 wa SADC uliofanyika Madagascar: "Kuimarisha Viwanda, Mapinduzi ya Kilimo, Mabadiliko ya Nishati kwa SADC Inayostahimili Misukosuko," wakisisitiza kuwa uchumi imara wa kikanda unategemea amani ya nchi wanachama.

Mkutano huo uliendeshwa na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, aliyekuwa Mwenyekiti wa kikao, na ulihudhuriwa na wakuu wa nchi na wawakilishi kutoka mataifa 15 ya SADC.

Viongozi walipongeza Tanzania kwa kuendeleza misingi ya amani na wakasema mchakato wa maridhiano unaoendelea ni mchango muhimu kwa uthabiti wa eneo lote la Kusini mwa Afrika.

# Mfumo wa bila riba watajwa nyenzo muhimu ya ujumuishaji kifedha

Mkurugenzi Mtendaji wa Soko la Hisa la Nigeria (NGX) Limited, Jude Chiemeka, amesema fedha zisizo na riba (non-interest finance) ni njia muhimu ya kuwajumuisha watu wengi zaidi kwenye soko la mitaji na kukuza uchumi wa nchi.

Akizungumza kwenye Mkutano wa 7 wa Kimataifa wa Fedha za Kiislamu Afrika (AICIF) uliofanyika Lagos, Chiemeka alisema fedha za aina hii hutoa nafasi kwa wawekezaji wanaotaka uwekezaji wa kimaadili na usiokiuka kanuni za dini.

Kwa kuliona hilo, alisema ndiyo sababu NGX imeunda Non-Interest Finance Board, jukwaa maalumu la bidhaa zinazokubaliana na Sharia, ili "kufungua mtaji wa kimaadili, kupanua fursa za uwekezaji na kuendesha maendeleo endelevu."

Kwa njia ya ubunifu na ushirikiano, alisema, Nigeria inaweza kujipambanua kama kitovu cha fedha za Kiislamu barani Afrika.

Kwa mujibu wa Business Post Nigeria, soko la mitaji lisilo na riba nchini limekua kwa kasi, likichochewa na hati fungani za serikali (sovereign Sukuk) ambazo sasa zimefikia zaidi ya N1.4 trilioni kwa miradi mbalimbali ya miundombinu. Mwenyekiti wa NGX Group, Umaru Kwairanga, alisema ubao huo maalumu wa NGX unatoa nafasi kwa Sukuk, mifuko ya uwekezaji ya Kiislamu na hata ETF zisizo na riba, ili kuvuta wawekezaji wanaotaka uwazi na ujumuishaji.

## Mafunzo benki bila riba yaamsha hamu kupokea sekta hiyo Ghana

**Takriban washiriki 400 kutoka taasisi za fedha, benki, mashirika ya uwekezaji na wanafunzi wa masuala ya fedha wamejiunga na warsha ya mtandaoni iliyoandaliwa na Chartered Institute of Bankers (CIB) Ghana kuhusu benki zisizo na riba (non-interest banking), ikiwa ni juhudi za kuielimisha sekta ya fedha kuhusu mbinu mbadala na jumuishi za utoaji huduma.**

**Warsha hiyo ililenga kufafanua misingi ya benki zisizo na riba – inayojulikana pia kama benki za Kiislamu – ikiwamo kuepuka riba (interest), kugawana faida na hasara, na kuwekeza kwenye shughuli halali kiuzalishaji.**

**Kwa mujibu wa tovuti ya News Ghana, wawezeshaji walibainisha kuwa bidhaa hizi zinaweza kutolewa kwa watu wa dini zote kwa sababu kiini chake ni maadili ya fedha, si dini pekee.**

**Viongozi wa CIB Ghana walisema mahudhurio makubwa yanaonyesha kuwa sekta ya fedha nchini iko tayari kupanua huduma kwa makundi ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakihofia au kuepuka mikopo ya kawaida kutokana na riba.**

**Walisisitiza kwamba benki zisizo na riba zinaweza kuwa nyenzo bora ya kuongeza ujumuishaji wa kifedha, kufadhili biashara ndogo na miradi ya miundombinu bila mzigo mkubwa wa riba.**

**Mada nyingine zilizoguswa ni namna ya kutunga sera za ndani za benki ili kuruhusu bidhaa za aina hii, udhibiti unaohitajika kutoka Benki Kuu, na fursa za kuvutia uwekezaji kutoka mashirika ya kimataifa yanayopendelea ufadhili wa kimaadili. Washiriki walipewa mifano ya bidhaa kama murabaha, ijara na sukuk ambazo tayari zinatumika katika masoko mengine ya Afrika.**

جُمادى أول

فتاوى

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Talaka, khului na haki za mume na mke

**Swali: Je, katika Uislamu Mke aliyetalikiwa anastahiki kugawana mali nusu kwa nusu na mwenza wake kwa sababu tu walikuwa mke na mume au anastahiki kipi?**

**Jawabu:** Swali lako ni zuri na linagusa masuala muhimu ya haki za kifamilia katika Uislamu.

Mosi, kuhusu kugawana mali baada ya talaka, katika Uislamu, mali ya mume na mali ya mke zinabaki kuwa za kila mmoja binafsi. Mke hastahiki kudai mgao wa mali kwa sababu tu waliishi ndani ya ndoa kama mke na mume au kwa sababu wametalakiana.

Qur'an Surat An-Nisaa (4), aya ya 32, inasema: "Wanaume wanafungu katika vile walivyochuma, na wanawake wanafungu katika vile walivyovichuma." Kwa hivyo, mali yoyote aliyoichuma mume kwa juhudi zake binafsi pasipo mchango wa mke ni yake, na vivyo hivyo kwa mke.

Pili, kuhusu stahiki za mke baada ya talaka, ni kwamba kulingana na hali ya talaka, kuna haki kadhaa ambazo mke anastahiki kwa mujibu wa Sharia:

- Mahari: Ikiwa mke hajalipwa mahari yake yote wakati wa kufunga ndoa, mume anapaswa kumalizia sehemu ya mahari hiyo iliyosalia wakati wa uhai wake au kumaliziwa na warithi wake baada ya kufa kwake.
- Kutoa matumizi wakati wa eda: Ikiwa ni talaka ya kwanza au ya pili (talaka rejea), mume anawajibika kumpa matumizi mtalaka wake kipindi chote cha eda ambacho ni twahara tatu, hedhi tatu, au miezi mitatu ikiwemo. Mahitaji hayo ni pamoja na chakula, makazi, mavazi, nk.
- Kutoa matunzo kwa watoto: Kama wapo watoto, mume anawajibika kugharamia mahitaji yao yote ikiwemo (chakula, mavazi, karo zao za elimu, makazi nk). Huduma hizo kwa watoto zitaendelea hata baada ya talaka.
- Kitoka nyumba au kumfariji mtalaka baada ya talaka: Qur'an Surat Al-Baqara (2), aya ya 241 pia imetaja kuwa ni sunna (na kuna baadhi ya wanazuoni wanaona ni wajibu) mume kumpa mke aliyemuacha zawadi au kwa lugha nyingine kitoka nyumba kama sehemu ya kumfariji na kukumbuka hisani: "Na wanawake walioachwa wapewe cha kuliwaza kwa mujibu wa sharia hii ni haki ya wajibu kwa wacha Mungu..."

Tatu, kuhusu "wanandoa kugawana mali", kwenye baadhi ya nchi zisizo za Kiislamu, sheria za kiraia zinatamka wazi kuwa mali iliyopatikana wakati wawili hao wamo ndani ya ndoa inastahiki kugawanywa nusu kwa nusu. Hilo ni suala la kisheria za nchi (civil law), si la kidini.

Lakini, kwa mujibu wa Sharia ya Kiislamu, mgao huo hauko isipokuwa kama, kwanza, mke alishiriki moja kwa moja katika kuchuma mali (mfano, walifanya biashara ya pamoja), au iwapo mume mwenyewe ameridhia kumpa mtalaka wake sehemu ya mali hiyo.

Nne, na mwisho: Kwa mujibu wa Uislamu: Mke hastahiki kugawana mali kwa sababu tu aliishi na mume ndani ya ndoa. Mke anastahiki mahari yake kamili, matumizi na matunzo kipindi cha eda, matunzo ya watoto (kama wapo) na kitoka nyumba cha kumfariji (mut'ah).

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Naomba kuelimishwa kuhusu tofauti kati ya talaka na khului (au mke kuomba kuvunja ndoa kwa kulipa fidia)?**

**Jawabu:** Umeuliza swali muhimu sana. Hakika kuelewa tofauti kati ya talaka na khului, ni jambo la msingi sana katika fiqhi ya ndoa na hasa linapokuja suala la haki za mali na matunzo baada ya kuvunjika kwa ndoa.

Mosi, hebu tuangalie kwa utaratibu, tukianza na maana ya misamiati hii miwili tukianza na talaka kisha khului.

Talaka ni kitendo cha mume kumwacha mke wake kwa kauli, maandishi au kitendo maalum kinachaoshiria talaka. Hii ni haki aliyopewa mume na Sharia, lakini anapaswa kuitumia kwa haki, hekima na kwa sababu za msingi.

Khului, kwa upande wake, ni aina ya kuvunjika kwa ndoa kunakoombwa na mke na mume akaridhia ambapo mke anarudisha mahari au sehemu ya mali aliyopewa kama fidia ili aachwe.

Qur'an imeutaja utaratibu huu kwenye Surat Al-Baqara (2) aya ya 229: "...Wala si halali kwenu kuchukua kitu chochote mlichowapa wake zenu, isipokuwa wote wawili wakihofia ya kwamba hawawezi tena kutimiza mipaka ya Allah. Basi mkihofia hivyo, basi si dhambi kwa wote wawili ikiwa mke atajikomboa kwa kitu (fidia). Hii ni mipaka ya Allah; basi msikiuke. Na watakaoikiuka mipaka ya Allah, hao ndio madhalimu"

NA MWANDISHI WETU

# Hatari kwa afya kutokana na maduka ya dawa kuuza dawa bila cheti cha daktari

**Utafiti wa kimataifa uliyochapishwa katika The Lancet ulionyesha kuwa usugu wa viuavijasumu ulihusishwa na vifo vya watu milioni 4.71 duniani, ambapo takriban asilimia 24 ya vifo hivyo vilitokana moja kwa moja na usugu wa dawa**

Mwelekeo unaoongezeka wa maduka ya dawa nchini Tanzania kuuza dawa, hasa viuavijasumu, bila cheti cha daktari unaibua wasiwasi mkubwa miongoni mwa wataalam wa afya ya umma.

Wanaonya kwamba tabia hiyo ikiachwa iendelee bila kudhibitiwa inaweza kugeuka janga kubwa la kiafya. Awali, maduka ya dawa yalikusudiwa kutoa dawa kwa mujibu wa maagizo ya kitabibu pekee, lakini sasa yamegeuka kuwa vituo visivyo rasmi vya matibabu ambako wagonjwa hupata dawa bila kumwona daktari.

Kwa mujibu wa Baraza la Famasi Tanzania, dawa kama vile za kutibu malaria aina ya Artemether–Lumefantrine (ALU) na viuavijasumu kama Amoxicillin na Doxycycline zimeorodheshwa kuwa za kupewa kwa cheti cha daktari pekee. Hata hivyo, hali halisi ni tofauti — Watanzania wengi sasa hutegemea maduka ya dawa kwa uchunguzi na matibabu, mara nyingi bila kwenda hospitalini kabisa.

Ingawa urahisi huo ni wa kuvutia, wataalam wanaonya kuwa madhara yake ni makubwa, mojawapo likiwa ni ongezeko la usugu wa viuavijasumu (AMR) — hali ambapo bakteria, virusi na vijidudu vingine hubadilika na kushindwa kudhibitiwa na dawa zilizoundwa kuviua.

## Tatizo la kimataifa na la ndani

Utafiti wa kimataifa uliyochapishwa katika The Lancet ulionyesha kuwa usugu wa viuavijasumu ulihusishwa na vifo vya watu milioni 4.71 duniani, ambapo takriban asilimia 24 ya vifo hivyo vilitokana moja kwa moja na usugu wa dawa. Iwapo hatua hazitachukuliwa, wataalam wanatabiri kuwa vifo vinavyohusiana na AMR vitaongezeka kwa asilimia 70 kufikia mwaka 2050, huku Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ikitarajiwa kuathirika zaidi.

Hapa nyumbani, utafiti uliofanywa, ulionyesha kuwa asilimia 89 ya wafanyakazi wa maduka ya dawa hutoa viuavijasumu kwa wagonjwa wa maambukizi ya njia ya mkojo bila cheti cha daktari, huku asilimia 87 wakikiri kutoa dozi pungufu kulingana na dalili tu za mgonjwa, bila vipimo vya maabara.

Jaribio dogo lililofanyika Sinza, Dar es Salaam, lilithibitisha jinsi hali hiyo imeenea. Mwandishi aliingia duka la dawa akijifanya ana dalili za kisonono; bila cheti cha daktari, alipewa sindano na dawa na kuambiwa aende duka lingine ili asidungiwe. Mtoa huduma alikiri kuwa "anaogopa" kudunga mwenyewe. Katika duka jingine, dawa kamili ya malaria ilipewa baada ya kuelezea dalili za homa pekee. Kati ya maduka 30 yaliyotembelewa, 20 yalitoa dawa bila kuuliza cheti wala historia ya matibabu.

Baadhi ya wahudumu walidai kuwa na mafunzo yasiyo rasmi ya kitabibu waliyojipatia hospitalini wakati wa mafunzo kwa vitendo, ambayo sasa hutumia kuwashauri wateja.

Mmoja alisema: "Baada ya chuo nilifanya field hospitalini, nikajifunza kusaidia wagonjwa. Ndivyo ninavyofanya sasa."

Mwingine alisema tabia hiyo husababishwa pia na wateja wenyewe: "Mara nyingi mgonjwa anasisitiza kwamba daktari alimuambia anunue dawa. Kwa kuwa nataka kuuza, namtimizia haja."

# Shirkah yataja hisa za Twiga Cement, Swissport kukidhi vigezo halal DSE

Kampuni ya usimamizi wa uwekezaji wa Kiislamu, Shirkah Asset Management, imetoa ripoti yake ya robo ya tatu ya mwaka 2025 ikionyesha kuwa kati ya hisa zote za Soko la Hisa la Dar es Salaam zilizo chini ya uangalizi wao wa sharia, zilizobaki kuwa halal ni mbili pekee: Twiga Cement na Swissport.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, hisa za Twiga zimepanda kwa asilimia 52.78 tangu Januari 2025, huku Swissport ikipanda kwa asilimia 42.73, na kufanya Shirkah Halal Index kufikia ukuaji wa jumla wa asilimia 50.23 mwaka huu.

Shirkah imeeleza kuwa hisa za Vodacom Tanzania na TOL Gases bado "hazijarudi kuwa halal", hivyo wawekezaji wametakiwa kuendelea kuzitenga kwa mujibu wa mapendekezo ya sharia.

Kwa upande wa masoko ya kimataifa ya halal, ripoti imeonyesha kuwa S&P 500 Shariah Index imekua kwa 16.35%, FTSE Shariah Emerging Index kwa 20.5%, huku FTSE/JSE Sharia Top 40 ya Afrika Kusini ikiongoza kwa ongezeko kubwa la 71.6% katika randi ya Afrika Kusini.

Katika taarifa hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirkah, Salum Awadh, amesema kampuni imekamilisha mkataba na kampuni ya udalali ya AIB–AXYS Africa ili kuwawezesha wateja wa Shirkah kuwekeza kwenye Soko la Hisa la Nairobi na masoko mengine ya ukanda huo.

Wakati huo huo, Shirkah imepanga kuanzia robo ya nne 2025 hadi robo ya kwanza 2026 kuzindua mifuko minne ya halal: Shirkah Hisa Fund, Shirkah Sukuk Fund, Shirkah REIT na Shirkah Commodities Fund, hatua iliyowekwa wazi kuwa inasubiri kukamilika kwa leseni za wadhibiti.

Mpango mwingine uliotajwa ni kurudisha Shirkah Halal Startups Incubator kusaidia biashara changa zinazofuata sharia, pamoja na uzinduzi wa Shirkah NUNUA Fund ambayo itatoa ukwasi kwa miamala ya soko la pili. Shirkah pia imekaribisha taasisi na mfuko wa waqf kujiunga na mpango wake mpya wa uwekezaji wa taasisi, Shirkah Corporate PRE.

## Kenya yafungua ubalozi mdogo Jeddah

**Serikali ya Kenya imezindua Ubalozi Mdogo (Consulate General) mjini Jeddah, Saudi Arabia, hatua inayolenga kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kulinda maslahi ya maelfu ya Wakenya wanaoishi na kufanya kazi katika eneo la Magharibi mwa Saudi Arabia.**

**Kwa mujibu wa tovuti ya habari ya The Eastleigh Voice News, uzinduzi huo uliongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje, Korir Sing'oei.**

**Ubalozi huu mpya utasaidia kazi za ubalozi uliopo Riyadh kwa kutoa huduma karibu na miji mitakatifu ya Makka na Madina, ambako Wakenya wengi hupita kwa ajili ya Hajj na Umrah. Pia utashughulikia masuala ya ajira, migogoro ya wafanyakazi wa nyumbani na ulinzi wa Wakenya walioko Jeddah na maeneo ya jirani, jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu.**

**Sing'oei alisema hatua hiyo ni sehemu ya mpango wa Kenya kupanua uwepo wake Mashariki ya Kati na kufungua fursa zaidi za biashara, utalii, elimu na uwekezaji kati ya Nairobi na Riyadh.**

## Msikiti wa Jamia, Nairobi waadhimisha miaka 100

**Msikiti wa Jamia jijini Nairobi umeadhimisha miaka 100 tangu msingi wake uwekwe Septemba 7, 1925 kwa uzinduzi wa kitabu maalumu na kutangaza kubadili sura ya kituo chake cha televisheni cha Kiislamu kuwa Jamia TV.**

**Katika hafla ilihudhuriwa na Waziri wa Afya Aden Duale, viongozi wa msikiti na waumini, imeandika tovuti ya The Eastleigh Voice News.**

**Kitabu hicho, "Jamia Mosque Nairobi 100-Year Journey" kilichoandikwa na Ghalib Yusuf Tamim, kinaeleza historia ya msikiti huo kuanzia ujenzi wake uliokamilika 1933, usanifu wake, upanuzi na mchango wake kwa Waislamu na jiji la Nairobi.**

**Katika maadhimisho hayo, Kamati ya Msikiti ilitangaza pia kuibadilisha Horizon TV kuwa Jamia TV pamoja na nembo na mwonekano mpya ili kuimarisha Da'wah na vipindi vya malezi, elimu na maisha ya Kiislamu.**

UKHTI FATIMA SS

# Si Uislamu tena...mrengo wa kulia tishio kubwa zaidi la kigaidi Ulaya

Serikali ya Uingereza imesema watu wengi waliotajwa kwa hatari ya kuingia kwenye msimamo mkali mwaka uliopita walikuwa wale wanaofuatilia siasa kali za mrengo wa kulia, na si wale wanaohusishwa na itikadi za Kiislamu kama ilivyozoeleka.

Watu hao, kupitia mpango wa serikali uitwao 'Prevent' unatumika kugundua mapema watu wanaoanza kuonyesha tabia au mawazo yanayoweza kuwapeleka kwenye ugaidi, halafu kuwasaidia kabla hawajafanya tukio.

Kwenye mwaka ulioishia Machi 2025, watu 8,778 waliripotiwa kwenye mpango huu – hii ni idadi kubwa kuliko miaka yote 10 iliyopita. Kati ya hao, watu 1,798 (asilimia 21) waliripotiwa kwa sababu ya "siasa kali za mrengo wa kulia" – kama chuki kali kwa wageni au kauli za kibaguzi.

Watu 870 tu (asilimia 10) walihusishwa na itikadi za Kiislamu zenye msimamo mkali. Wengi zaidi – karibu nusu na bila shaka sio Waislamu – walikuwa hawana itikadi maalumu, ila walionekana tu wanaelekea kwenye vurugu.

Kundi jingine la watu 469 (asilimia 5) lilipelekwa Prevent kwa sababu walionekana kuvutiwa na vurugu kubwa au mashambulio ya watu wengi, hata bila kufuata imani au siasa maalum. Idadi ya kundi hili imeongezeka sana katika miezi ya mwisho.

Serikali imesema kuongezeka kwa taarifa hizi kumetokea baada ya tukio baya la Southport mwaka 2024 ambako watoto watatu waliuawa kwenye darasa la dansi, tukio lililowafanya watu kuwa makini na vijana wanaopenda vurugu.

Ripoti pia imeonyesha kuwa karibu theluthi moja ya walioripotiwa walikuwa na changamoto za afya ya akili au walikuwa kwenye wigo wa tawahudi (autism). Wale wanaoonekana wako kwenye hatari zaidi hupelekwa mbele kwenye kamati maalum (Channel) ambako hupewa ushauri au msaada ili wasielekee kwenye ugaidi. Wengi wa wanaosaidiwa ni watoto wa miaka 11 hadi 15.

## Wabunge Uingereza: Serikali itambue tatizo la Islamofobia

**Kundi la wabunge 40 wa Chama cha Labour na wabunge huru limeitaka serikali ya Uingereza kuidhinisha rasmi tafsiri ya Islamophobia, baada ya takwimu kuonyesha makosa ya chuki dhidi ya Waislamu yameongezeka karibu asilimia 19 katika mwaka uliopita.**

**Barua hiyo, iliyoandikwa na Mbunge Afzal Khan na kutumwa kwa Waziri wa Makazi, Jamii na Serikali za Mitaa, Steve Reed, imetiwa saini na wabunge miongoni mwao Diane Abbott, Dawn Butler, Kim Johnson na Andrew Gwynne, ikieleza kuwa mwaka 2025 takribani asilimia 45 ya makosa ya chuki za kidini yaliwalenga Waislamu.**

**Barua hiyo iliyonukuliwa na gazeti la Guardian la Uingereza, imesisitiza kuwa makosa ya chuki dhidi ya Uislamu yamepanda jumla ya asilimia 92 tangu 2023, hivyo serikali ichukue "hatua muhimu" ya kuweka ufafanuzi wa chuki dhidi ya Waislamu.**

**Serikali ilianzisha Februari mwaka huu kikosi kazi cha kuandaa maelezo ya kile kinachotafsiriwa kama matendo yasiyokubalika, ubaguzi, chuki na mashambulizi dhidi ya Waislamu au wanaodhaniwa kuwa Waislamu. Taarifa inaeleza kuwa kikosi kazi hicho, kinachoongozwa na wakili Dominic Grieve KC na kuhusisha wataalamu wakiwemo Akeela Ahmed na baronesi Shaista Gohir, tayari kimekabidhi ripoti yake kwa waziri na serikali "inaichunguza".**

**Wabunge hao wanataka tafsiri hiyo iidhinishwe wakati wa mwezi wa uhamasishaji dhidi ya Islamophobia mwezi Novemba na kwa ushirikiano na jumuiya za Kiislamu ambazo zinapaswa kulindwa. Serikali za zamani za Conservative zilikuwa na wasiwasi kuwa tafsiri za awali zingezua hofu ya kufifisha uhuru wa kujieleza, lakini ripoti za awali zimeeleza kuwa pendekezo jipya litahifadhi haki ya kuikosoa dini.**

**Msemaji wa Wizara ya Makazi na Jamii amesema idara "inaangalia kwa makini mapendekezo ya kikosi kazi na itajibu wakati muafaka."**

UKHTI FATIMA SS

# Walowezi wa Kiyahudi washambulia wakulima Wapalestina msimu wa mavuno

Wakulima wa Kipalestina Ukingo wa Magharibi wameripoti wimbi jipya la mashambulizi na vitisho kutoka kwa walowezi wa Kiyahudi wakati wa msimu wa kuvuna mizeituni ili kuwazuia kuingia kwenye mashamba yao.

Kwa mujibu wa taarifa ya CNN iliyochapishwa Ijumaa, mashambulizi hayo yamehusisha kupigwa, kuvunjwa magari, kuchomwa au kukatwa miti ya mizeituni na kuondolewa kwa wakulima kwa nguvu.

Taarifa za mashirika mengine huru zinaonyesha taswira hiyo hiyo. Umoja wa wakulima na wanaharakati waliopo mashambani unasema baadhi ya vijiji, hasa karibu na maeneo ya walowezi kama Turmus Ayya, As-Sawiya na maeneo ya kaskazini ya Nablus, wakulima wamelazimika kurudi nyumbani wakiwa hawajavuna chochote kwa sababu kuingia shambani "ni sawa na kuhatarisha maisha."

Guardian iliripoti kwamba hadi asilimia 70 ya mizeituni ya mji mdogo wa As-Sawiya haifikiki bila kuhofia makabiliano na walowezi au jeshi la Israel.

Mashirika ya kufuatilia ukatili wa walowezi yanasema zaidi ya mashabulizi 150 yalirekodiwa katika wiki za kwanza za msimu wa mavuno mwaka huu, yakijumuisha pia kuchoma mamia ya miti ya mizeituni na kuwafukuza wanaharakati wa Israeli na wa kigeni waliokuja kuwalinda wakulima.

Olive ni uti wa mgongo wa kiuchumi kwa maelfu ya familia za Kipalestina: inatumiwa nyumbani, inauzwa kama mafuta na inahifadhiwa kama urithi wa ardhi.

Ripoti za mashirika ya misaada na ya Umoja wa Mataifa zimeonya kwamba ukataji na uchomaji wa miti ya mizeituni una athari ya muda mrefu kwa kipato cha wakulima na pia unawaondolea Wapalestina uwepo wa kudumu kwenye ardhi yao.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa kwa Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu (OCHA) ilisema zaidi ya Wapalestina 3,200 wamelazimika kuondoka makazi au maeneo ya malisho tangu 2023 kwa sababu ya ukatili wa walowezi na vizuizi vya kwenda mashambani.

CNN imeripoti kuwa katika baadhi ya matukio wanajeshi wa Israel walikuwepo lakini hawakuingilia kati, jambo ambalo mashirika ya haki za binadamu yamelieleza kama mazingira ya "kutokuwapo kwa adhabu" kwa walowezi – hoja ambayo imewahi kuripotiwa pia na vyombo vingine vya habari kuhusu msimu wa mavuno wa miaka iliyopita.

Makundi ya Wapalestina na wanaharakati wa Israeli wanaopinga ujenzi wa makazi yameitaka serikali ya Israel kuwapa wakulima ulinzi wa moja kwa moja wakati wa msimu wa mavuno na kuwafikisha mahakamani wanaoharibu miti ya mizeituni, wakisema bila hatua hizo "mavuno yataendelea kuwa uwanja wa vurugu kila mwaka."

## Muislamu atajwa shujaa Uingereza kwa kumdhibiti muuaji kwenye treni

**Mfanyakazi Muislamu raia wa Algeria amepongezwa kwa ujasiri wake baada ya kuzuia muuaji kuongeza idadi ya waathirika kwenye shambulio la visu ndani ya treni mkoani Cambridgeshire, Uingereza, tovuti ya 5 Pillars imeripoti.**

**Mfanyakazi huyo, Samir Zitouni (48), ambaye amekuwa akifanya kazi na Kampuni ya London North Eastern Railway (LNER) kwa zaidi ya miaka 20, alijeruhiwa vibaya Jumamosi jioni (1 Novemba) wakati aliposimama katikati ya mshambuliaji na abiria wengine kwenye treni iliyokuwa ikitoka Doncaster kwenda London King's Cross. Polisi walisema picha za CCTV zinaonyesha Zitouni akimzuia mshambuliaji kusogea mbele na hivyo "bila shaka kuokoa maisha ya watu wengi."**

**Zitouni ni miongoni mwa watu 11 waliolazwa hospitalini kutokana na shambulio hilo, na Polisi wa Usafiri wa Uingereza wamesema hali yake ni "mbaya lakini imetengamaa." Waziri wa Uchukuzi, Heidi Alexander, pia alimsifu na kumtaja kama "mwenye ujasiri wa ajabu."**

**Mshukiwa, Anthony Williams (32), amefikishwa katika Mahakama ya Peterborough akikabiliwa na mashitaka 10 ya kujaribu kuua kuhusiana na tukio hilo. Polisi walisema hawamtafuti mtuhumiwa mwingine. Wafanyakazi wenzake LNER na viongozi wa jamii wamemtakia Zitouni nafuu ya haraka, wakisema kitendo chake ni cha kujitolea kupita kiasi.**

## KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Dunia ipaze sauti kulaani hujuma za Israel huko Gaza

Mapema wiki iliyopita, Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki, Hakan Fidan aliikosoa Israel akisema kuwa inakiuka makubaliano ya kusitisha mapigano na Hamas, hivyo amelitaka Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kujadili mipango ya kutuma kikosi cha kimataifa cha kuleta uthabiti huko Gaza.

Fidan aliyasema hayo baada ya kumalizika kwa mkutano kati ya wanadiplomasia kutoka Mataifa ya Kiarabu na mengineyo, uliofanyika Novemba 3, 2025 jijini Istanbul, Uturuki.

Makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya Israel na Hamas yalianza kutekelezwa Oktoba 10, 2025, lakini Israel bado inaendelea kushambulia maeneo ya Gaza ikiishutumu Hamas kwa kukiuka makubaliano ya usitishaji vita, chini ya 'Mpango wa amani wa Gaza' ulioandaliwa na Rais Trump mwezi uliopita.

Haipingiki na ndivyo ilivyo, kwamba, mpango huu unakusudia kuunda taifa bandia la Palestina lisilo na mipaka inayoeleweka, lisilo na madaraka yoyote katika mambo ya ulinzi na usalama, diplomasia au uhamiaji. Ni mpango wa kupora ardhi ya Ukingo wa Magharibi, ambao hadi sasa unakaliwa na walowezi wa Kiyahudi takriban 600,000.

Mpango huu unalenga kuifanya Palestina iwe nchi ambayo mambo yake yote yanaamuliwa na Israel. Kwa mujibu wa maazimio ya Umoja wa Mataifa na sheria ya kimatifa, Palestina inatakiwa iwe na mipaka iliyokuwapo kabla ya Israel kuvamia Ukingo wa Magharibi mwaka 1967. Mji mkuu unatakiwa uwe Jerusalem ya Mashariki (Al–Quds).

Badala yake, Trump anataka Palestina iwe na kitongoji kidogo kama 'mji mkuu' nje ya Jerusalem. Wapalestina wanaambiwa: "Mkipenda mnaweza kuuita Jerusalem Mashariki.".

Kibaya zaidi, Trump ameipa Israel uhalali wa kuvamia maeneo ya Ukingo wa Magharibi wa Mto Jordan, maeneo ambayo Israel iliyavamia mwaka 1967. Tangu wakati huo, walowezi kutoka Israel wamekuwa wakihamia huko na kujenga makazi haramu ya kudumu kinyume na sheria ya kimataifa.

Anachokifanya Trump ni kujaribu kuunda taifa la Palestina lisilo na sifa za utaifa chini ya himaya ya majeshi ya Israel. Uporaji wowote wa ardhi – uwe wa asilimia 50 au 10 katika Ukingo wa Magharibi ni kinyume cha sheria. Itoshe kusema hivyo.

Hivi sasa Israel inatoa kisingizio cha 'Hamas kuchelewesha kwa makusudi kukabidhi miili ya mateka wao' ili kuhalalisha mauaji ya raia katika Ukanda wa Gaza, wakati mateka hao waliuawa na kufukiwa kwenye vifusi vya majengo yaliyobomolewa na makombora ya majeshi yao wenyewe.

Hii ni ishara ya ubaguzi wa rangi na chuki za kupindukia walizonazo viongozi wa Mazayuni dhidi ya Wapalestina. Ni vyema basi mataifa yakabeba dhima ya msingi na wajibu wa kuishinikiza Israel iache kuwaua raia wa Gaza, kuharibu nyumba zao, na kupora ardhi na mali zao.

Hujuma za Israel dhidi ya watu wa Gaza haziathiri Palestina pekee, bali pia mataifa yote ya Kiarabu na Kiislamu, hivyo kuna haja ya kuungana na kupinga hujuma zao kupitia shinikizo la kiuchumi, ikiwamo kusitisha kuwauzia mafuta na kukata uhusiano wa kidiplomasia.

Tofauti za kisiasa na madhehebu zisizuie juhudi za kupinga 'uchokozi wa Mazayuni' katika Ukanda wa Gaza.

UKHTI FATIMA SS

# Dubai yazindua kampeni ya "Matendo Bilioni 1 ya Wema"

Dubai imezindua kampeni kubwa ya kimataifa inayoitwa "1 Billion Acts of Kindness" (Matendo Bilioni 1 ya Wema), yenye lengo la kuwahamasisha watengenezaji maudhui (content creators) duniani kuonyesha na kusambaza matendo ya huruma na kusaidia jamii.

Kampeni hii imezinduliwa kwa ushirikiano kati ya mkutano maarufu wa 1 Billion Followers Summit na mtengenezaji maudhui mashuhuri duniani, MrBeast (Jimmy Donaldson) huku ikisaidiwa pia na Mohammed Bin Rashid Al Maktoum Global Initiatives (MBRGI) na Varkey Foundation.

Wazo la kampeni ni rahisi: watu wanaotengeneza video mtandaoni wafanye kitendo cha wema katika jamii zao – kama kusaidia wazee, watu wenye ulemavu, wasio na makazi, kupanda miti, au kufanya harambee za kuchangia wahitaji – kisha wapige video na kuituma. Lengo ni kukusanya matendo haya hadi yafike bilioni 1 duniani.

Kwa mujibu wa tovuti ya Gulf News, ushiriki uko wazi kwa watengenezaji maudhui kutoka nchi yoyote. Wanatakiwa kutuma video zao kabla ya Desemba 1, 2025 kupitia fomu rasmi ya mtandaoni kwenye tovuti: 1billionsummit.com/mrbeast, na kutumia hashtagi #1BKindness na #1BillionSummit. Video zitapimwa kwa uhalisia, ubunifu, namna ilivyosimuliwa na athari chanya kwa jamii.

Video 10 zenye athari kubwa zaidi zitatajwa kwenye mkutano wa nne wa 1 Billion Followers Summit utakaofanyika Dubai tarehe 9–11 Januari 2026. Washindi hao watafanya kazi moja kwa moja na MrBeast na timu yake kutekeleza matendo makubwa zaidi ya wema yatakayorekodiwa na kusambazwa duniani.

Viongozi wa mpango huu wamesema lengo ni kuonyesha kwamba maudhui ya mitandaoni yanaweza kutumika kwa mambo ya kibinadamu, si burudani pekee. Wamesisitiza pia kuwa hata tendo dogo la wema linaweza kuanzisha mabadiliko makubwa endapo litasambazwa na watu wengi. Kampeni hii inatarajiwa kuwafikia mabilioni ya watu kwa sababu mkutano wa 2025 uliwakutanisha wanaoitazama zaidi ya watu bilioni 2.3 mtandaoni.

جمادى أول

MAKALA MAALUM

NA SHEIKH SEIF RUGA

# Haki tano zinazohusu mali ya marehemu

Allah Mtukufu ameumba ardhi, mbingu na vilivyomo, kisha akaumba uhai na kifo ikiwa ni ishara na alama ya uwezo wake. Kila kiumbe kilichopo ulimwenguni kitakufa, na Allah pekee ndiye atakayebaki milele, hafi, na ndiye Mbora wa warithi wote.

Katika mtazamo wa Uislamu, mambo ya mwanadamu hayaishii baada ya kifo chake, bali kuna masuala anayohusiana nayo baada ya umauti, nayo ni kurithiwa mali alizoacha. Haki zinazohusiana na mali ya urithi ni miongoni mwa haki zisizoweza kupuuzwa.

Katika sheria ya Uislamu, mali ya urithi inahamishwa kwa warithi baada ya mwenye mali kufariki. Hata hivyo, mali hiyo haiwi ya warithi peke yao bali kuna mambo mengine yanayohusiana nayo. Ikiwa mali ya marehemu inatosha kutekeleza haki zote, basi hutolewa yote; na kama haitoshi ni lazima ipangiliwe kwa utangulizi kulingana na vipaumbele.

Wanazuoni wa sheria ya Kiislamu (Al–fuqahau) wamekubaliana kuhusu mpangilio wa haki hizi isipokuwa kwenye mambo machache madogo waliyotofautiana, kama tutakavyojadili hapa chini.

### Mosi, haki zinazohusiana na mali wakati mtu akiwa hai

Kiuhalisia, mali hizi si katika mali zilizoachwa na marehemu kwa sababu zilikuwa zimeambatana na mali alizokuwa anamiliki kabla hajafariki. Mfano wake ni kama haki ya mtu aliyeweka rehani kitu chake kwa marehemu kabla ya kufa, n.k. Haki hizi huitwa madeni yanayohusiana na mali yenyewe (Ain At–Trika).

Kwa mujibu wa Jopo la wanazuoni wa sheria ya Kiislamu kutoka madhehebu ya Hanafi, Malik na Shafi ni kwamba, haki hizi hutangulizwa kulipwa kabla ya gharama za maziko. Kwa upande wa madhehebu ya Hanbali, kipaumbele chao ni kutoa gharama za maziko kwanza kabla ya madeni.

Jopo la wanazuoni waliotanguliza kulipa madeni kwanza, wamesema madeni yanayohusiana na mali ya marehemu yalikuwepo hata kabla ya kifo, na maandalizi ya mazishi yalikuja baada ya kifo. Kwa hiyo, haki ya deni inatangulia kabla ya gharama za mazishi.

Kwa upande wao, wanazuoni wa Kihanbali wamesema kuwa maandalizi ya gharama za mazishi ni mahitaji ya lazima kwa heshima ya marehemu. Katika kipindi cha uhai, mtu hutanguliza mahitaji yake ya msingi kabla ya madeni, hivyo hata baada ya kifo ni lazima maandalizi yatanguliwe kabla ya deni.

### Pili, baada ya kulipa haki zinazohusiana na mali

Haki hizi, kwa maana yake halisi zinaitwa 'At–Tarika', na jumla yake zipo nne. Haki hizi zinapewa kipaumbele kwa mpangilio ufuatao. Kwanza ni haki ya maandalizi ya mazishi, ikiwamo kumuosha, kumvisha sanda, kumswalia, kumzika n.k.

Kiwango cha maandalizi na gharama za mazishi ni sharti kilingane na matakwa ya sheria ya Kiislamu. Sheria haikubali kutumia mali ya marehemu katika mambo ya kimila au desturi zinazopingana na sheria ya Kiislamu, kwani fedha hizo ni haki ya watu wengine (warithi, wanaomdai marehemu na walioachiwa usia).

### Tatu, madeni

Hizi ni haki zilizokuwa zinamlazimu marehemu, lakini hazihusiani moja kwa moja na mali maalum. Madeni haya yamegawika sehemu mbili. Kwanza, madeni ya Allah ambayo mfano wake ni zaka ambazo marehemu hakutoa wakati wa uhai wake, malipo ya makosa ya kisheria (kafara), na nadhiri ambazo hakuzitekeleza.

Jopo la wanazuoni wa Kiislamu (Jumhur Al–Ulamaa) limesema, madeni haya ni lazima yalipwe kabla ya wasia na kugawa mirathi, kwa kauli ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Deni la Allah linastahili zaidi kulipwa."

Lakini wanazuoni wa madhehebu ya Hanafi wamesema kuwa deni hilo linabatilika kwa kufariki mhusika. Hata hivyo rai hii imekosolewa kwa kuwa iko kinyume na ushahidi wa andiko.

Aina ya pili ni madeni ya watu. Haya ni madeni aliyoyaacha marehemu kwa watu, mfano mahari, malipo ya huduma au mishahara ya watu aliyowaajiri, mikopo, n.k. Madeni haya yanalipwa kutoka kwenye mali yake kwa kuzingatia usia aliyouacha au baada ya kuhakiki madeni anayodaiwa.

### Nne, wasia (kumpa mtu haki ya kitu au manufaa yake baada ya kufa)

Wasia unatekelezwa kwa masharti mawili. Mosi, wasia utoke katika theluthi (1⁄3) ya kilichosalia baada ya kulipa madeni na gharama za maziko, siyo kutoka katika theluthi ya mali yote. Kama wasia utakua zaidi ya theluthi (1⁄3), basi utatekelezwa tu kwa ridhaa ya warithi.

Pili, wasia usitolewe kwa mrithi, kwa kauli ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake): "Hakuna wasia kwa mrithi." Wanazuoni wamekubaliana kuwa deni hutangulizwa kabla ya wasia, kama ilivyokuja katika kauli ya Ali bin Abi Twalib (Allah amridhie) kwamba: "Mtume wa Allah alihukumu kuwa deni hutangulizwa kabla ya wasia."

Ama kauli ya Allah Ta'ala ya kutanguliza wasia kisha deni: "Baada ya kutekelezwa wasia au deni." [Qur'an, 4:12], wanazuoni wameeleza kuwa wasia umetangulia kabla ya deni ili kuwahimiza warithi wasiupuuze, kwani hakuna anayedai wasia kama linavyodaiwa deni.

### Tano, urithi

Baada ya kutekelezwa haki zote zilizotajwa hapo juu, mali iliyobaki hugawanywa kwa warithi wanaostahiki, kwa mujibu wa viwango vilivyotajwa katika Qur'an Tukufu na Sunna.

جُمادىٰ أُول

**NASAHA ZA WIKI**

NA YUSUFU AMINI
0787 503 085

# Mtume alizingatia Akhera, sisi twakumbatia dunia

"Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na pumbao, na pambo, na kujifaharisha baina yenu, na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake, kisha hunyauka ukayaona yamepiga manjano kisha yakawa mabua. Na Akhera kuna adhabu kali na maghfira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe zidanganyazo." [Qur'an, 57:20].

"Na maisha ya dunia si chochote isipokuwa ni mchezo na pumbao. Na bila shaka Nyumba ya Akhera ni bora zaidi kwa wachamungu. Je, basi hamtii akilini." [Qur'an, 6:32].

Haya ni maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yanayotukumbusha kuwa, dunia hii tuliyopo ni sehemu bandia ya kuishi na siku moja itafikia ukomo wake. Kwa hiyo, ni vizuri kuchukua hatua kwa kutathmini muda tunaoupoteza hapa duniani katika mambo maovu na ya upuuzi, kwani muda wetu una thamani na maana kubwa katika maisha ya Akhera.

Kuhusu hali ya maisha ya Akhera, Mtume (rehema na amani iwe juu yake) ametwambia: "Lau mngeyajua yale ninayoyajua (mimi), basi mngecheka kidogo na mngelia sana (kutokana na adhabu za Akhera)." [Sahih Bukhari].

Ni ukweli usio na shaka kwamba, wengi wetu siku hizi hatuna muda wa kutekeleza mambo ya dini yetu. Hali hiyo inatokana na mihangaiko mingi na shughuli za kidunia, ambazo humsababishia mwanadamu uchovu wa mwili na akili, na kumfanya apanue wigo wa kupenda mambo mazuri na anasa za dunia.

Siku hizi kila mmoja yuko 'bize' na kutafuta 'maisha mazuri' ya dunia, utajiri, wadhifa (cheo), na kustarehe kwa aina mbalimbali za burudani. Haikatazwi kushughulika na dunia, bali kilichokatazwa ni mtu kuwa mtumwa wa dunia na anasa zake, kiasi cha kusahau lengo la kuumbwa kwake (kumuabudu Mwenyezi Mungu).

Qur'an yatuambia: "Na tafuta kwa yale aliyokupa Mwenyezi Mungu makazi mazuri ya Akhera, wala usisahau sehemu yako ya dunia." [Qur'an, 28:77]. Kumbe basi, kilicho muhimu ni kutafuta maisha ya Akhera kwa wingi bila kuisahau dunia.

Ilivyo ni kwamba, mwanadamu akiipenda sana dunia na anasa zake huisahau Akhera. Ni vigumu kwa mtu aliyetopea katika anasa na starehe za dunia kukumbuka maisha ya Akhera, hasa pale anapotafuta mali kwa njia za haramu. Hali hii inapojitokeza na kadiri muda unavyozidi kusonga, mtu hukimbilia mambo machafu na maovu na hatimaye moyo wake hutawaliwa na maasi.

Imam Nawawi (Allah amrehemu) alinukuliwa akisema kuhusu maisha ya dunia: "Mapigo ya moto ya mtu yanamwambia: Hakika maisha ni dakika na sekunde. Basi inyanyue nafsi yako baada ya mauti yako. Kutajwa kwako ni kama kutajwa kwako mara ya pili."

Naam! Hiyo ndiyo hali halisi ya maisha yetu – kama ulijenga nyumba nyingi duniani, siku utakapozikwa utasifiwa na watu kwamba umeipamba dunia kwa nyumba nyingi za kifahari; lakini itakuwa ni hasara kwako ikiwa hujaijenga Akhera.

Kwa hiyo, Muislamu unatakiwa kukumbuka kwamba hakuna atakayekujengea makazi mema baada ya kufa isipokuwa wewe mwenyewe. Usishughulishwe sana na dunia ukakosa hamasa ya kuijenga Akhera, kwani maisha ya Akhera ni ya milele na ya kudumu zaidi.

Epuka kupoteza muda wako katika mambo/vitu ambavyo havina faida ya kidunia wala Akhera, na elekeza hisia zako kwa Mwenyezi Mungu peke yake na si kwenye vitu au watu wengine. Kufikia hatua hiyo, ni lazima tujitenge mbali na hadaa pamoja na starehe za dunia, ambazo kwa kiasi kikubwa humfanya mtu aghafilike na kumtii Mwenyezi Mungu.

## Mafanikio ya kweli

Ushawahi kujiuliza ni jambo gani litamfanya mtu kuvuna mafanikio ya Siku ya kiyama? Je, ni elimu kubwa, utajiri au marafiki wengi? Laa hasha. Mafanikio ya kweli ni kutumia umri wako katika kumuabudu kikamilifu Mwenyezi Mungu, kwa mujibu wa Sunna (hadith) sahihi za Mtume (rehema za Allah na amani iwe juu yake).

Ili kujua ni mambo gani yanafanyika kwa kufuata Sunna za Mtume na kujua mambo yaliyozushwa (bid'a), inatubidi kuisoma dini ya Allah Ta'ala kutoka kwenye vyanzo salama na vya kutegemewa ndani ya Ahlu Sunnat Wal–jama'ah. Lakini ili Sunna ya Mtume ituokoe, ni lazima tuitekeleze kwa kufuata mwongozo (manhaj) ya sawasawa kwa mujibu wa wema waliotangulia.

Afya Pure Drinking water

"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com

جمادى أول

SEHEMU YA 4

MUSSA IMANI
SHEHA,
ZANZIBAR
0773 181 494



# HUDHAYFA BIN AL-YAMAN: Mtunza Siri za Mtume

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Hudhayfa (Allah amridhie) alishiriki katika vita mbalimbali pamoja na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie). Vilevile alishiriki, baada ya kufariki Mtume, harakati mbalimbali za ukombozi na kuifungua miji na kueneza Uislamu katika kipindi cha makhalifa Abubakr, Umar na Uthman (Allah awaridhie).**

**Katika maisha yake, Hudhayfa bin Al-Yaman (Allah amridhie) alijipamba na uchamungu, ukweli, uaminifu, na alikuwa na wingi wa ibada. Alimhofu sana Allah na adhabu Zake.**

**Katika moja ya simulizi zake anasema: "Watu (Maswahaba wenzangu) walikuwa wakiuliza kuhusu mambo ya kheri, ama mimi nilimuuliza Mtume kuhusu mambo ya shari ili nisije nikayatenda bila ya kujua.".**

### Kuteuliwa kuwa gavana

Katika utawala wake, Umar (Allah amridhie) alimteua kuwa gavana wa Madain (Iraq). Katika barua aliyowatumia watu wa huko na kuondoka nayo aliandika: "Nimekuleteeni kiongozi makini, muadilifu, naomba mumsikilize, mumtii na mumpe kila msaada atakaowaombeni."

Hudhayfa alitoka akiwa amepanda punda wake. Alipofika na kuwasomea agizo la Umar wakasema: "Tuombe chochote unachokitaka tutakupatia." Akawaomba chakula cha kumkimu tu.

Hudhayfa alipokuwa huko alifanya mambo mengi ya kimaendeleo na ustawi wa Uislamu, ikiwemo kuipiga Nahawand mnamo mwaka wa ishirini na mbili (22) Hijriya na kuishinda, kisha kufunga mkataba wa amani na viongozi wake.

### Maradhi na kifo chake

Hudhayfa alipatwa na maradhi akiwa Iraq. Hali ilipokuwa ngumu, baadhi ya Maswahaba walimtembelea nyumbani mwake katikati ya usiku. Akawauliza: "Saa ngapi sasa?" Wakasema: "Tuko karibu na alfajiri." Akasema: "Najikinga kwa Allah na asubuhi ya kunipeleka motoni," kayasema hayo mara mbili.

Kisha akawauliza: "Mmekuja na sanda?" Wakasema: "Ndio, ipo." Akawaambia: "Msizifanye ghali sanda na za gharama, ikiwa nina kheri yoyote mbele ya Mola wangu Allah atanibadilishia (nguo) nzuri zaidi."

Baada ya maneno hayo aliomba na kusema: "Ewe Mola wangu, hakika Wewe ndiye Ujuwaye kwamba mimi (katika maisha yangu yote) nilipenda ufakiri kuliko utajiri, na nikapenda hali ya chini kuliko fahari, na napenda kifo kuliko uhai." Kisha roho yake ikatolewa.

Hudhayfa alikufa mwaka wa thalathini na sita huko Madain, Iraq, siku arubaini baada ya kuuawa Uthman (Allah awaridhie). (Taz: Suwarun min Hayat Swahaba, uk. 306).

### Tujifunzayo kupitia maisha ya Hudhayfa

Kuna mengi ya kujifunza katika maisha ya Swahaba huyu mtukufu. Miongoni mwa hayo ni umuhimu wa kutunza siri za watu. Siri ni amana. Ziwe za ndoa, kazini, ndani ya taasisi za dini, na zile za jamaa na marafiki – zote zinatakiwa zihifadhiwe.

Tunajifunza namna Maswahaba walivyokuwa watiifu kwa Mtume na jinsi walivyojitolea katika kuutetea Uislamu. Hayo tunayapata katika tukio la usiku wa Khandaq. Simulizi ya Swahaba huyu aidha, inatutaka tuipende zaidi Akhera, na tuache tamaa za kupindukia katika kuyapata maisha bora ya hapa duniani.

Tunamuomba Allah amridhie Hudhayfa bin Al-Yaman na Maswahaba wengine wote. Na sisi Atufishe tukiwa Waislamu wa kweli, na Atukutanshe nao siku ya hesabu. Aamin.

JUNAYNAT ALLY DAMA

# WHO na msukumo mpya kwa tiba asili kuelekea mkakati wa afya jumuishi 2025-2034

Shirika la Afya Duniani (WHO) limerejea mezani na mjadala mzito kuhusu tiba asili baada ya karibu nusu karne. Mnamo 7 Novemba 2025, WHO kupitia Bulletin of the World Health Organization ilitoa toleo maalum kabisa kuhusu tiba asili, ikiwa ni mara ya kwanza tangu 1977 kufanya jambo kama hilo.

Toleo hili limekuja kama maandalizi ya Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa Tiba Asili utakaofanyika New Delhi, India kuanzia 17–19 Desemba 2025, na linaonyesha wazi kwamba ulimwengu sasa unatambua tena nafasi ya tiba za jadi katika kujenga mifumo imara na jumuishi ya afya.

Sababu ya mjadala huu kufufuliwa ni rahisi: mabilioni ya watu duniani bado wanategemea tiba asili kama mlango wao wa kwanza wa kupata huduma za afya. Kwa wengine, ni chaguo la kitamaduni na kiimani; kwa wengine, ni kwa sababu huduma za kisasa ziko mbali au ni ghali.

WHO inaeleza kwamba mahitaji haya yataendelea kukua, na hata sekta pana ya "wellness" inayohusiana na tiba na mitindo ya maisha ya kiafya inatarajiwa kupanda kutoka dola trilioni 5.6 mwaka 2022 hadi dola trilioni 8.5 ifikapo 2027. Hii inaonyesha kuwa tiba asili si jambo la pembezoni tena, bali ni eneo la kiuchumi, kiafya na kisera linalohitaji mwongozo.

Hata hivyo, kuna tatizo kubwa: ushahidi wa kisayansi haujaenda sambamba na matumizi. WHO inaonya kwamba chini ya asilimia 1 ya fedha za utafiti wa afya duniani ndizo zinazoelekezwa kwenye tiba asili.

Hii inaleta pengo – mataifa yanataka kuingiza tiba asili kwenye mifumo yao ya afya ya msingi, lakini hawana data ya kutosha kuthibitisha usalama, dozi, mwingiliano wa dawa, au namna bora ya kuunganisha mbinu za jadi na tiba za kisasa. Ndiyo maana WHO imeandaa Global Traditional Medicine Strategy 2025–2034 ili kusaidia nchi zinazoendelea na hata zilizoendelea kutengeneza mifumo iliyo "people-centred," salama na yenye ushahidi.

Toleo la Bulletin halikujikita tu kwenye nadharia. Lilibeba makala za utafiti asilia, mapitio ya kimfumo, makala za sera na maoni ya wataalamu kuhusu masuala nyeti kama haki za wenyeji na maarifa asilia, ulinzi wa mali miliki (intellectual property), mgawanyo wa manufaa, na hata matumizi ya akili bandia (AI) katika kuorodhesha, kuchanganua na kuhifadhi maarifa ya jadi.

Ujumbe hapa ni kwamba tiba asili si "mchanganyiko wa majani" pekee, bali ni mfumo wa maarifa ulioounganishwa na mazingira, jamii na utambulisho wa watu. Kuuheshimu mfumo huu ni suala la haki za binadamu na pia la uendelevu wa mazingira.

Mkutano wa New Delhi wa Desemba 2025 umepewa kaulimbiu "Restoring balance: The science and practice of health and well-being." Kauli hii ni muhimu kwa sababu inafunga pengo kati ya wanasayansi na wahifadhi wa tiba za jadi. WHO inataka kuona si tu tiba za jadi zinatumiwa, bali zinatumiwa kwa usalama, zimepitiwa na kanuni, na zinawanufaisha wale waliobeba maarifa hayo tangu jadi.

Ndiyo maana ajenda ya mkutano itagusa kanuni na udhibiti, ulinzi wa bioanuwai (kwa kuwa dawa nyingi hutoka kwenye mimea), mazungumzo ya heshima na jamii za kiasili, pamoja na fursa mpya zinazotokana na teknolojia. Pia, WHO inasisitiza suala la mgawanyo wa manufaa. Mara nyingi maarifa ya tiba asili yamechukuliwa, yakasindikwa, na baadaye bidhaa kuuzwa bila jamii husika kunufaika. Kupitia mijadala ya sasa – sambamba na mazungumzo ya kimataifa kuhusu mfumo wa kugawana vimelea na manufaa (pathogen access and benefit sharing) – kuna dhamira ya kuhakikisha kwamba taarifa za kiafya na za kijeni zinaposhirikiwa, basi faida zake zinabaki kuwa za pamoja, si za kampuni chache tu.

MAKALA MAALUM

NA SHEIKH SEIF RUGA



# Malezi ya mtoto wanandoa wanapotengana

Lengo kuu la sharia ya Kiislamu ni kutimiza manufaa na kuzuia madhara. Sharia hii tukufu imehakikisha haki za watu binafsi na jamii nzima za binadamu. Miongoni mwa uzuri wa sharia ya Kiislamu ni kulinda haki za wanyonge, yakiwamo makundi maalumu kama watoto.

Kwa ajili yao, Uislamu umeweka kanuni za jumla pamoja na sharia maalumu zenye maelezo ya kina, zikiwamo sharia za malezi na utunzaji wa mtoto (Al–Hadhana). Malezi katika Uislamu ni miongoni mwa mambo mazuri sana yaliyomo katika sharia hii tukufu.

Wanazuoni wa zamani na wa sasa wa sharia ya Kiislamu (Al–fuqahau) wametofautiana katika kueleza maana ya malezi kwa maneno, ingawa maana yao kimsingi ni moja. Baadhi ya wanazuoni wa Kishafi wameyaelezea malezi kuwa ni kumuangalia na kumtunza yule asiyeweza kutofautisha mambo au kujisimamia, kwa kumlea katika yale yanayomfaa na kumlinda dhidi ya mambo yanayoweza kumuangamiza.

Kumlea mtoto mdogo, kumtunza na kusimamia mambo yake ni jukumu la wajibu la wazazi wawili wanapokuwa kwenye ndoa. Lakini mama ana nafasi kubwa zaidi katika haki ya malezi, kwani mara nyingi ndiye anayebeba jukumu la malezi kwa huruma na upendo.

Baba ana nafasi lakini ni ndogo zaidi kulingana na wajibu wa kijinsia na kimaumbile. Allah Mtukufu ameutaja wajibu huu ndani ya Qur'an: "Na useme: Ee Mola wangu, warehemu wazazi wangu kama walivyonilea utotoni." [Qur'an, 17:24]. Aya hii tukufu inaonesha wazi kuwa malezi ni jukumu la lazima la wazazi katika kipindi cha utotoni.

Hata hivyo, iwapo wazazi watatengana (kwa talaka), suala la nani anayepewa haki ya kulea mtoto linaibuka; je, ni mama au baba? Na je, haki hiyo inamhusu mtoto wa kiume au wa kike?

## Haki ya malezi kipindi cha talaka

Malezi na utunzaji wa mtoto unakuwa kwa wazazi wote wawili iwapo ndoa yao bado ipo. Wanazuoni wote wamekubaliana kuwa, iwapo wazazi (baba na mama) wakitengana kwa talaka malezi ya mtoto yanakuwa ni haki ya mama na jukumu la baba ni kumhudumia.

Siku moja Mtume (rehema na amani ziwe

juu yake) alimwambia mwanamke ambaye alitalikiwa, kisha mumewe akataka kumchukua mtoto aliyezaa naye: "Wewe (mke) una haki zaidi ya kumlea mtoto maadamu hujaolewa."

Hivyo, kauli hii ya Mtume wa Allah ni hukumu ya lazima inayopaswa kutekelezwa. Iwapo mama ataolewa na mume mwingine ambaye si baba wa mtoto, basi haki hiyo itaondolewa kwake.

Imam Bukhari (Allah amrehemu) amenukuu hadith ya Al–Barrau bin Azib kuhusu haki ya kumlea binti wa Hamza (Allah amridhie). Ali (Allah amridhie) alisema: "Mimi nina haki zaidi naye, kwani yeye ni binti wa ami yangu", huku Ja'far akisema: "Ni binti wa ami yangu, na mama yake mdogo ni mke wangu." Naye Zaid akasema: "Yeye ni binti wa ndugu yangu."

Mtume wa Allah akahukumu mtoto huyo kwenda kulelewa kwa mama yake mdogo, akasema: "Mama yake mdogo ni kama mama mzazi." Hadith hii inaonesha uhalali wa malezi kwa mama mdogo, na kwamba wakati wa mgogoro ndiye anapewa kipaumbele kuliko ndugu wengine wa karibu wa mtoto.

Aidha, miongoni mwa athari (kauli za Masahaba wa Mtume) zilizopokewa kuhusu jambo hili, ni simulizi inayomhusu Umar (Allah amridhie) ambaye alimtaliki mkewe wa Kiansar baada ya kuzaa naye mtoto aitwaye Asim.

Baada ya mwanamke huyo kuolewa tena na mume mwingine, mtoto alilelewa na bibi yake mzaa mama. Umar (siku moja) alipokutana na mtoto wake barabarani alimkumbatia kwa mapenzi, lakini bibi yake mzaa mama alizozana na Umar na kumdai mtoto huyo, wakapeleka shauri hilo kwa Khalifa Abubakar As–Swiddiq (Allah amridhie), naye akahukumu mtoto abaki kwa bibi yake mzaa mama.

## Masharti ya malezi

Miongoni mwa masharti ya malezi ni; mosi mwenye kulea awe mtu mzima, kwani mtoto mdogo hawezi kumlea mtoto mwenzake. Pili awe na akili timamu; tatu awe na uwezo wa kulea vizuri na nne awe mwadilifu na mwaminifu katika malezi.

Kuwa Muislamu siyo sharti la msingi katika malezi kwa sababu huruma ya asili kwa mtoto haipotei kwa tofauti ya dini, isipokuwa kama kuna hofu kwamba mtoto ataathiriwa na ibada za dini nyingine.

Kwa ujumla, wanawake wana haki zaidi ya malezi kuliko wanaume, na malezi hayo huanza tangu mtoto anapozaliwa. Hata hivyo, muda wa mwisho wa kulea mtoto kwa mwanamke baada ya ndoa kuvunjika unatofautiana kati ya madhehebu ya Kiislamu.

Kwa mujibu wa madhehebu ya Kishafi, malezi huendelea kwa mtoto – awe wa kiume au wa kike hadi anapofikia umri wa kutambua mambo (utambuzi). Kwa kawaida, umri huu unakadiriwa kuwa kati ya miaka saba hadi minane. Mtoto akifikia umri huu hupewa haki ya kuchagua kuishi na mmoja kati ya wazazi wake, na akimchagua mmoja basi hukabidhiwa kwake.

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Muombeni Allah awaepushe na mitihani

Zaid bin Thabit (Allah amridhie) amehadithia kuwa, siku moja walikuwa na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) kwenye bustani ya Banu Najjar, Mtume akiwa juu ya mnyama wake akawaelekea na kuwaambia: "Mtakeni Allah ulinzi kutokana na fitina mbalimbali zilizo wazi na zilizofichikana." ***[Muslim].***

## Mafundisho ya hadith

Allah ametupa mitihani ya kheri na shari ili wadhihiri wavumilivu wanaoweza kusimama imara wakati wa mitihani (fitina), na wabainike wale ambao ni dhaifu katika kumtii Allah. Mitihani hii ni ya aina mbaimbali na inaweza kuja kwa njia ya kheri au shari. Wapo waliopewa mali ikawa ni mtihani kwao, lakini pia wapo waliopewa ufukara ikawa ni mtihani kwao.

Watoto na afya pia ni mtihani, ukiwa navyo au ukivikosa. Mathalan, huenda maradhi yakakuingiza katika shirk, na ukiwa na afya njema unaweza kujikuta unaitumia katika kumuasi Allah. Anasema Allah: "Kila nafsi itaonja mauti; na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na kwetu Sisi mtarejeshwa." [Qur'an, 21:35].

Kutokana na kukabiliwa na mitihani hii, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) ametufundisha tumuombe Allah atulinde na fitina mbalimbali.

## Lazima tutahiniwe

Allah anauliza: "Hivi watu wanadhania kuwa wataachwa hivihivi tu kwa kusema kuwa tumeamini bila wao kufitinishwa (kupewa mitihani mbalimbali). Na kwa hakika tuliwafitinisha wale waliokuwepo kabla yao. Allah atawatambua wale ambao ni wakweli na atawatambua waongo." [Quran, 29:2–3].

Mitihani ni utaratibu wa Allah kwa sisi waja wake, kwani hata kaumu (umma) zilizotangulia zilipewa mitihani ya kila namna ili kupimwa imani yao. Leo hii tupo katika mapambano na fitina kubwa mno ambazo zimewafunika watu kama vile kipande cha usiku wa giza.

Fitina hizo ni pamoja na mali, watoto, wanawake, marafiki, ajira, n.k. Baadhi ya fitina hizi zinatupelekea kuchanganyika na waovu (marafiki wabaya), kulingania na kuitangaza batili (kama sehemu ya ajira, mathalan watangazaji wanaopigia debe kamari na pombe), kupiga vita haki na maasi mengine mbalimbali.

Mwanadamu anapokumbwa na matatizo hutokea moja kati ya mambo mawili – aidha hujikomboa na tatizo, jambo ambalo kila mwenye akili anapaswa kulifanya, au hukata tamaa na kujisalimisha moja kwa moja katika matatizo hayo hadi akaangamia. Hii ya pili si tabia ya wenye akili na wenye kujitambua.

Hili la kutojitambua na kupelekea kujisalimisha moja kwa moja katika fitina za kilimwengu, ndiyo mwelekeo wa watu wengi hivi sasa. Watu wamezama katika dimbwi la fitina hizo na hawaoni hatari, athari na madhara makubwa, jambo ambalo linatishia mustakbali wa maisha yao ya Akhera.

Fitina ni nyingi na zina kasi na nguvu kama mawimbi ya bahari. Ni wachache mno wanaosalimika na fitina hizi. Hivyo basi, ni wajibu wetu kuchukua tahadhari na kushikamana na mwongozo wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) ili tusalimike.

## Kutangazwa wazi kwa fitina

Kuna wanaohubiri maovu ya aina mbalimbali na itikadi potofu, wakiwamo wabunifu wa matangazo ya ulevi, uzinzi, riba na mengineyo. Hawa wanatumia nyenzo mbalimbali, mfano vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na kila fursa wanayoipata kuhakikisha kuwa ujumbe unawafikia wengi.

Hivi sasa maasi yanafanyika waziwazi, na imefikia hatua watu wameyazoea na hawaoni kama ni kitu cha ajabu kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na wale wanaohubiri maasi. Yeyote anayejitokeza kupinga maasi hayo yaliyozoeleka anaonekana ni kichekesho mbele za watu.

## Tuchukue tahadhari

Muislamu achukue tahadhari kubwa ili asiwe miongoni mwa wenye kuiamsha fitina na wala asijiingize kwenye fitina hizi zilizomzunguka.

Haya yote yalitabiriwa na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) aliposema: "Kutatokea fitina ambayo mtu aliyekaa kitako atakuwa bora kuliko aliyesimama, na aliyesimama atakuwa bora kuliko anayetembea, na anayetembea humo atakuwa bora kuliko anayekimbia. Atakayajitokeza kuingia katika fitina hizi basi zitamuangamiza. Kwa hiyo yeyote atakayepata mahali pa kujikinga au kimbilio basi ajikinge kwayo." [Bukhari na Muslim].

Ni vema tukanasihiana juu ya fitina hizi kwani fitina huleta maangamivu. Allah anatuonya kwa kusema: "Na jikingeni na fitna ambayo haitowasibu waliodhulumu peke yao kati yenu. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu." [Qur'an, 8:25]. Na maana ya neno 'Jikingeni', ni kuamrishana mema na kukatazana maovu na tusipofanya hivyo basi adhabu itakapokuja itatufikia sote.

IDARA YA DAAWA

## Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

www.islamicftz.org

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Namna ya kusaidia watoto kuzishinda hofu zao

Watoto wote hupitia vipindi vya hofu wanapokua. Wengine huogopa giza, wengine wanyama, wengine majanga, na watoto wakubwa huanza kuogopa kushindwa shuleni au kutengana na marafiki. Hofu yenyewe si tatizo; tatizo huwa ni namna watu wazima wanavyoitikia hofu hiyo. Mzazi, mlezi au mwalimu anapojua kuitikia kwa upole na maarifa, hofu ya mtoto hupungua na mtoto hujifunza stadi muhimu ya maisha: "naogopa, lakini naweza kujidhibiti."

## Mosi, sikiliza na kubali hisia zake

Hatua ya kwanza ni kumsikiliza mtoto kwa makini anaposema, "Ninaogopa," hata kama sababu inaonekana ndogo na ya kijinga. Kwa mtoto, hofu hiyo ni halisi. Ukimwambia, "Ah, hayo ni ya kitoto," au ukacheka, ataacha kukueleza na hofu itajificha ndani. Hata zingeongezeka hofu za vitu vingine hatosema. Mpe nafasi aeleze alichoona, alichosikia au alichofikiri.

## Pili, tambua kwamba hofu za kufikirika nazo ni za kweli kwao

Mtoto anaweza kuogopa "jini chumbani" au "mdudud kwenye kabati." Ni rahisi kusema halipo, lakini ni bora kusema: "Naona unaogopa. Hebu tuangalie pamoja." Mnapochunguza, akili yake inapata taarifa mpya: mzazi yuko upande wangu, na tunaweza kukabiliana na hilo. Pia, ukimuua mdudu, inampa Faraja kuwa hatari haipo tena.

## Tatu, mpe maarifa sahihi

Hofu nyingi hutokana na kutokujua. Mtoto akihofia radi, angalia vitabu, picha au video rahisi vya kueleza kuwa radi ni sauti ya umeme angani. Ufafanuzi unapotolewa kwa lugha rahisi, ubongo hupunguza hofu kwa sababu sasa unaelewa chanzo. Ni hivyohivyo iwapo mtoto atamuogopa mzungu, mmasai au polisi. Maelezo sahihi na rahisi yanaweza kufuta hiyo hizo.

## Nne, mpe faraja na uwe karibu zaidi kwa muda

Hofu nyingi hupita ndani ya wiki au miezi michache, kwa hiyo kipindi hicho mtoto anahitaji ukaribu, ratiba inayojirudia na maneno ya kutuliza. Zidi kusoma hadithi jioni, kaa chumbani hadi alale, muonyeshe kuwa nyumbani kuna usalama. Uthabiti wako leo ndiyo ujasiri wake kesho.

## Tano, muelekeze kwa Mungu

Imani humsaidia mtoto ajue kuwa hata kama hupo naye, yupo Mwenyezi Mungu pamoja naye muda wote na anayeweza kumuomba ulinzi. Aambiwe kuwa Mwenyezi Mungu ana huruma, ameumba kila kila kitu, tajiri, ana nguvu juu ya kila kitu na muhimu zaidi anapenda mno kuombwa. Mtoto akijua kuwa kwenye kona yake kuna Mola wake, akamtegemea kisawasawa, ataweza kushinda hofu zake.

## Sita, tumia mbinu za maandalizi na uigizaji

Kama unajua kutatokea jambo linaloweza kumtisha — kuhama, kukaa na dada wa kazi, kwenda hospitali — mtayarishie mapema. Mcheze "tunaenda kwa daktari," mtembeze kwenye nyumba mpya kabla hamjahamia, au mfanye "upekuzi wa wadudu" kabla ya kulala. Mazoezi haya humpa hisia ya udhibiti.

## Saba, ongeza usalama wa kihisia

Wakati wa hofu, ongeza muda wa familia na mtoto, mikumbatio na maneno chanya: "Wewe ni shujaa... hata ukiogopa bado tunakupenda." Hakikisha wazazi wote wanatumia ujumbe uleule ili mtoto asichanganyikiwe.

## Mambo yasiyofaa kufanya

Miongoni mwa mambo ambayo hayafai kufanya ni pamoja na kumwambia "wewe ni mwoga." Hii inaumiza na inaongeza aibu. Pia, usiache hofu tu "iishe yenyewe" bila kuzungumza — kwani hofu nyingine hukua na kuwa wasiwasi hadi ukubwani.

Jambo jingine la kutofanya ni kumlinganishe na ndugu yake au watoto wengine: "Kaka yako haogopi!" Kulinganishwa kunamuadhiri na kujisikia kushushwa thamani, jambo lnaloweza kuleta athari kisaikolojia.

UKHTI FATIMA SS

# Saikolojia ya ulaji: tunakula zaidi au tofauti kuliko tunavyodhani

**Wengi wetu huamini tunakula kwa sababu tuna njaa au kwa kuwa mwili unahitaji nguvu. Lakini watafiti wa ulaji kama Dkt Brian Wansink wanaonesha kuwa uamuzi wa chakula ni wa mara kwa mara kuliko tunavyofikiri: mtu anaweza kufanya zaidi ya maamuzi 200 ya chakula kwa siku na asilimia kubwa yake hutokea bila kujua.**

**Hapa ndipo saikolojia ya ulaji inapojitokeza – nguvu iliyojificha kutoka katika mazingira, hisia, utamaduni, harufu na sura ya chakula ambavyo vyote hivi hutuelekeza mezani.**

## Ukijaribu kufuta mawazo ya chakula, unayazidisha

Ubongo ukihisi unazuiliwa, hamu huongezeka, na matokeo yake kile ulichokatawa na ukifanikiwa kukiacha, unaporudi huwa unakula kupita kiasi. Hii ni kwa sababu akili zetu hupenda raha. Chakula si adui; ni chanzo cha starehe na kumbukumbu njema.

Njia bora ni kuruhusu uwepo wa vyakula unavyovipenda lakini uvifanye visiwe rahisi kuvifikia, na uongeze zaidi vyakula vyenye afya vinavyoonekana vizuri. Hii ndiyo "lishe usiyoitambua" – marekebisho madogo ya mazingira badala ya marufuku kali.

Majina na lebo za bidhaa huchora ladha akilini

Matarajio huathiri ladha. Utafiti mmoja uliwapa watu kinywaji kile kile lakini chupa zikaitwa majina tofauti. Walioambiwa ni kinywaji cha lebo Fulani kubwa waliiandika kuwa ni tamu zaidi na hata chakula chote kikaonekana bora. Hii huitwa expectation assimilation – kile tunachotarajia ndicho tunachokiona. Kwa hiyo ukijiambia mboga zako ni safi, zenye rangi na ladha, una nafasi kubwa ya kuzila bila kulalamika.

Macho huanza kula

Chakula kilichopangwa kwenye sahani nzuri, kikakatwa vizuri na kuoneshwa mbele ya macho kitaliwa haraka kuliko kile kilichofichwa kwenye mfuko wa nailoni. Hata nyumbani, tunda likiwa kwenye bakuli zuri mezani familia italikumbuka; likikaa ndani ya friji nyuma ya chupa za maji, na familia pia haitaligusa. Hivyo, onesha kwa kuremba vyakula vyenye afya na ficha visivyofaa.

Ukubwa wa sahani unaamua kiasi unachokula

Mtaalamu Wansink anaita mindless margin – tofauti ndogo ya takribani kalori 100 hadi 200 ambazo hatuzihisi. Ukipunguza sahani kwa asilimia 20 huwezi kutambua na ndiyo maana ukubwa wa sahani, kikombe au bakuli unaamua kiasi unachokula. Sahani kubwa "inakushawishi" ujaze zaidi; sahani ndogo hufanya ujisikie umemaliza hata kama kiasi ni kile kile. Hivyo, inashauriwa tumia sahani ndogo, pakua kiasi kabla ya kula, na usile moja kwa moja kutoka kwenye sufuria.

## Tunakula tunachokiona

Pipii, biskuti au chipsi vinapokuwa mezani na kuonekana kila unapopita, ubongo huchochea hamu hata kama hukuwa na njaa. Lakini ukivificha juu ya kabati au ndani ya droo, mwili husahau. Kinyume chake, ukiweka matunda tayari yameoshwa na kukatwa, utakula zaidi kwa sababu ni rahisi kuvifikia. Ugumu mdogo tu – kufungua friji, kupanda kiti, kufungua kifurushi – hupunguza ulaji holela.

Msukumo wa jamii

Ikiwa watu waliokuzunguka nao wanakula, huchangia kuamsha hamu ya kula. Tunapokuwa kwenye sherehe, vikao vya kazi au nyumbani na familia, tunajikuta tunachukua sahani ya pili kwa sababu wengine wamechukua, si kwa sababu bado tuna njaa. Huu ni msukumo wa kijamii. Vile vile, mila na desturi zetu hujenga tabia za ulaji: biriani Ijumaa, supu ya asubuhi nk.

Ladha hubadilika kulingana na muda na muktadha

Chakula hakina ladha ile ile siku nzima. Tumeliunganisha kichwani kwamba uji ni wa asubuhi, ugali ni wa mchana, na wali ni wa jioni. Ukipewa ugali na nyama saa 12 alfajiri unaweza kuikataa hata kama ni tamu. Hii ina maana mazingira na muda vinaathiri kukubali kwetu vyakula. Ukihitaji kubadili mlo—kwa mfano kula mboga zaidi—iweke kwenye muktadha unaoendana: iandae vizuri, ipe jina zuri, ije wakati ambao haionekani "nje ya wakati."

Hisia na ulaji

Mwisho, hisia zetu huchochea ulaji. Siku yenye msongo wa mawazo au upweke hutufanya tutafute chakula cha faraja: wali kwa nazi ya mama, chipsi, au ice cream. Huu si udhaifu bali ni hali ya ubongo kutafuta dopamine ya kutuliza. Njia bora ni kutambua hisia kabla ya kula. Ukifahamu chanzo, unaweza kuchagua chakula bora au kufanya kitendo kingine cha kutuliza kama kutembea au kunywa maji ya uvuguvugu.

Saikolojia ya ulaji inatuambia: hauko kwenye mapenzi mabaya na chakula, uko kwenye mazingira yanayokusukuma kula. Ukibadili kile unachokiona (sehemu, saizi ya sahani, majina ya vyakula), ukatambua hisia zako kabla ya kula, na ukaacha vita vya "sitawahi kula hiki," utaanza kula kwa njia ya akili zaidi. Mwili wako bado utapata raha ya chakula, lakini ubongo hautakuhujumu kisiri.

NA UKHTI FATIMA

Majanga kama mafuriko, moto, ugonjwa wa mlipuko, vurugu za kijamii au mabadiliko ya ghafla ya sera yanaweza kuipiga biashara chini siku moja tu.

Mara nyingi tatizo si kwamba mfanyabiashara ni mzembe, bali tukio lilikuja bila kutarajiwa, mauzo yakasimama lakini kodi, mishahara na madeni yakaendelea kukusanyika.

Habari njema ni kwamba biashara inaweza kusimama tena – lakini si kwa kubahatisha, bali kwa mpango.

Makala hii inajadili aina ya mipango inayoweza kusaidia biashara kusimama upya hatua kwa hatua.

Salimisha watu, mali

Awali ya yote, kwenye nyakati hizo za dharura, jambo muhimu ni kusalimisha kwanza, kisha hesabu hasara.

Kusalimisha ni kuhakikisha usalama wa watu na mali iliyosalia. Kisha fanya tathmini fupi lakini halisi: nini kimeharibika, nini bado kinafanya kazi, ni wateja gani bado wako hai, na ni madeni gani yanakukukaba.

Andika na hifadhi taarifa hizi zitakusaidia sio tu kwa mipango ya ufufuaji biashara bali pia kwa bima au msaada wa serikali/taasisi.

# Kurudi kwenye biashara baada ya janga: Mikakati, hatua kwa hatua

## Linda fedha iliyobaki

Majanga huwa yanaua biashara kwa kukata mtiririko wa fedha (cash flow). Hivyo hatua ya haraka ni unayoweza kuchukua ni kupunguza au simamisha matumizi yasiyo ya lazima; kuzungumza na mwenye pango au mkopeshaji uombe muda; na kulipa gharama muhimu zinazokufanya uendelee kufungua biashara (umeme, intaneti, leseni, mfanyakazi mmoja muhimu).

Lengo la kufanya haya ni kujijengea uwezo na stamina ya kuhimili wiki au miezi michache ya kujaribu kujenga upya.

## Wasiliana haraka na wateja wako

Biashara ikikaa kimya, wateja hudhani imekufa. Tuma ujumbe mfupi: "Tulikumbwa na mafuriko/moto lakini tunarudi. Kwa sasa tunatoa huduma hizi..."

Tumia WhatsApp broadcast, Instagram, mitandao, au hata simu binafsi kwa wateja wakubwa. Kwa kufanya hivi, unapanda mbegu ya mapato ya kwanza. Watu wengi huwa tayari kukusaidia ukionekana mkweli na unaendelea kupambana.

## Anza kidogokidogo

Usisubiri mpaka urejee kama zamani. Anza na kile kinachoweza kuuzwa leo. Kama ulikuwa na bidhaa 20, anza na 5 zinazozunguka haraka; na kama duka limeharibika, uza kwa mtandaoni au kwa kumpeleka mteja moja kwa moja.

Kama huna mtaji mkubwa, fanya pre-order (mteja alipe kwanza kisha unaleta) hii inakupa fursa ya kukuza mtaji. Kurudi hatua kwa hatua kunakupa fedha za kujijenga badala ya kukaa ukisubiri mkopo mkubwa usiojulikana utakuja lini.

## Tafuta vyanzo vya fedha vya kuvumilia majanga

Sio kila kurudi kunahitaji mkopo mkubwa wa benki. Kuna baadhi ya machaguo unaweza pia kuyazingatia ikiwemo vikundi vya kuweka na kukopa / SACCOS vya halali kwa mujibu wa sharia ya Kiislamu. Pia, unaweza kufanya mazungumzo na wasambazaji ya kukuongezea muda wa kulipia badala ya kulipa papo hapo. Pia, unaweza kufanya miradi midogo ya kukuongezea mapato ya haraka (kwa mfano, kuuza bidhaa za msimu wakati unarekebisha biashara yako kuu).

Ikiwa uliathiriwa na janga lililotangazwa, fuatilia mipango ya serikali/halmashauri au mashirika ya misaada yanayorejesha biashara ndogo. Lakini kumbuka: chukua fedha zinazoweza kulipika kwenye mapato halisi, si kwenye matumaini.

## Kuwa na mbadala wa wasambazaji

Biashara nyingi hushindwa kurudi kwa sababu chanzo chao kimoja cha bidhaa kimekatika. Tengeneza mpango mbadala. Mfano, muuzaji A akishindwa, uwe na chaguo B au hata C. Kama barabara zimeharibika, tafuta chanzo karibu. Kama bidhaa za nje zimekwama, tafuta mbadala wa ndani.

Ukifanya hivi, tukio jingine la janga la asili kama hilo likitokea kesho halitaangusha biashara yako kwa kiwango kilekile kwa sababu una mbadala.

## Sogeza biashara karibu na mteja

Majanga makubwa kama COVID yalitufundisha kwamba mteja anaweza asije dukani, lakini anaweza kununua. Hivyo weka namba ya WhatsApp kwenye maboksi/kurasa zako za mitandao ya kijamii, eka miundombinu ya kupokea malipo kwa simu; weka watu wako wa kukusambazia bidhaa kwa wateja.

Kadhalika, jitahidi kutangaza mara kwa mara kwamba "tunatoa huduma hata ikiwa..." kwa maana unaondoa sababu kama za umbali, mteja kukosa muda na kadhalika. Ukifanya biashara iwe rahisi kufikiwa, mapato yanarudi haraka.